# Nipashe

Alhamisi Mei 5, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580936

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SportPesa

TZS. 1,224,601,040

BET LEO UWE BILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Usahihi** kuhusu bei gesi kupikia katika masoko

UKURASA 2




**MULLER AONGEZA MKATABA BAYERN**

UKURASA 22



# Samia: Urais hauzoeleki

• **Ataja** mipango uendelezaji gesi, umeme, mambo aliyoyakabili, atoa dukuduku wanaosema anaupiga mwingi... *Endelea ukurasa 2*



Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 25 kwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile (wapili kulia), wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, jijini Arusha juzi. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa TEF, Bakari Machumu na Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Clocktower, Arusha, Emmanuel Kishosha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## IGP Sirro : 'Panya Road' wamenivunjia heshima

UKURASA 3

## Wachumi watoa angalizo kupanda bei ya mafuta

UKURASA 3


**MICHEZO** **PABLO AWASHUKIA MABEKI SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati mstari wa mbele), akiwa pamoja na kundi la wawekezaji kutoka nje ya nchi na baadhi ya viongozi wa wizara hiyo, baada ya kumalizika kwa kikao cha majadiliano kuhusu fursa na vivutio vya uwekezaji vinavyopatikana hapa nchini, jijini Dar es Salaam jana. (Watatu kulia mstari wa mbele) ni Balozi wa Norway hapa nchini, Elisabeth Jacobsen. **PICHA: WFM**

# Samia: Urais hauzoeleki

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema urais hauzoeleki kwa kuwa kuna mambo mengi na haamini kuwapo fundi kwenye nafasi hiyo.

"Au labda kwa sababu ya ugeni mwaka mmoja, lakini sidhani kama urais unazoeleka," Rais Samia alifafanua katika mazungumzo yake na Mkurugenzi Mkuu wa Azam Media, Tido Mhando, yaliyorushwa jana asubuhi.

Kuhusu uzoefu wake ulikofikia, Rais Samia alisema alijifunza kwa mtangulizi wake Rais John Magufuli stadi za kusimamia nidhamu ya kazi, inayojenga tija katika kuwajibika, jambo ambalo linamfanya hivi sasa kupata tafsiri sahihi ya kilichomfanya kuwa mkali kazini ili kupatikane matokeo chanya.

"Ukali wa maneno ninaweza nisiwe nao lakini kuna njia unazungumza na mtu anaelewa 'sasa mama amekusudia kuzungumza kitu'," alifafanua.

Anarejea hata alipoambiwa kubeba jukumu la kuongoza nchi kwa nafasi hiyo, alikiri kupata mshtuko lakini haukuwa wa kubeba majukumu, bali kilichosababisha ayabebe.

Rais anataja matatizo anayokutana nayo katika miradi mikubwa iliyoachwa na mtangulizi wake akiitekeleza, ni uwezo wa ndani kuiendesha, hata wakatumia mikopo.

UMEME

Rais Samia alifafanua tatizo la umeme nchini, akitaja kwamba mitambo mingi inayouzalisha imechakaa na mfumo wake ulikuwa haujakaa vizuri, hata kuhitaji maboresho.

"Bajeti ya mwakani tumeweka Sh. bilioni 500 ambazo tunakwenda kujenga kituo kikubwa cha kuimarisha umeme na kufanya usikatike katike," alisema.

Pia, kwenye bwawa la Mwalimu Nyerere, alisema kunafanyika tathmini maalum, tayari wameshaanza kuchukua dhidi ya ucheleweshaji wa mradi, matarajio ni kukamilika Juni mwaka 2024.

**MISHAHARA KUPANDA**

Kuhusu mishahara kupanda, alilitolea ufafanuzi kwamba mwaka jana ilipandishwa kimya kimya kuepuka wafanyabiashara kutumia fursa hiyo kupandisha bei za bidhaa.

"Hatukutamka watu watalalamika, watu hawaridhiki hawasemi kwamba serikali imesamehe moja, mbili, tatu, nne, tano kwa hiyo kwenye mishahara yetu kuna kitu kimebaki.

"Mpaka useme mshahara kima cha chini ni hizi pengine unaweza kutamka na isisaidie, ambapo kwenye bajeti hii tutakwenda nayo pia," alisema, huku akidokeza kodi ya mshahara haitoguswa.

**RIPOTI YA CAG**

Kuhusu ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Rais Samia alisema mengi yaliyoainishwa yamekwisha shughulikiwa na yaliyobaki yanafanyiwa kazi.

Alisema ripoti CAG imemfungua macho, akibaini Kitengo cha Ukaguzi katika Wizara ya Fedha na Mipango hakifanyi kazi yake inavyostahili, akitoa mfano hatua alizochukua kuhusiana na hilo ni kusafisha maeneo yenye dosari ikiwamo Mamlaka ya Bandari (TPA).

Pia aligusa kasoro chache zilizoonekana kwenye matumizi ya fedha za mkopo wa kukabiliana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19 kwamba tayari ameshachukua hatua, ikiwamo kuwafuta kazi wakurugenzi wanne.

**UHABA WA AJIRA**

Rais Samia aligusa kuhusu uhaba wa ajira, akirejea ripoti ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) inayobainisha asilimia 16 ya vijana duniani hawana ajira, naye serikali yake ikichukua hatua kadhaa kuziba pengo hilo.

Alizitaja kuwa ni ziara zake, akitumia mfano katika nchi za Marekani na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) zinazotarajiwa kuzaa ajira 800,000; ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi (VETA) vinavyowezesha vijana kujiajiri ikiendana kukuza ujuzi katika shughuli za kijamii na kufumua mtaala wa masomo uendane na mahitaji ya uchumi.

**GESI ASILIA**

Rais Samia pia alisema mazungumzo na wawekezaji katika uzalishaji wa gesi asilia yanaendelea vizuri na uzalishaji mkubwa unatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Vilevile, alifafanua kuhusu viongozi wanaomsifia kwamba 'anaupiga mwingi', akibainisha kuwa wapo wanaotamka hilo kutokana na uhalisia na wengine wanaotamka kwa malengo yao binafsi.

# Usahihi kuhusu bei ya gesi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA gazeti la Nipashe la Februari 24, 2022 kwenye ukurasa wa kwanza na wa pili, tuliochapisha habari yenye kichwa kisemacho 'Bei ya gesi sasa haikamatiki'.

Habari hiyo ilikuwa ripoti maalumu iliyoandikwa kwa kuangalia mwenendo wa bei ya gesi ya kupikia majumbani (LPG) katika mikoa mbalimbali nchini, kutokana na wananchi walivyoeleza kama walivyohojiwa na waandishi wetu.

Ripoti hiyo maalum iliyosawiri bei ya bidhaa hiyo kutoka katika kampuni mbalimbali zinazojihusisha na biashara hiyo, ilionyesha kuwa nishati hiyo imepanda na kuonyesha hali ya bei katika mitungi ya saizi tofauti. Miongoni mwa mikoa ambayo iliripotiwa bei kupanda ni Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Njombe na Mwanza.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, bei ya mtungi mdogo wa Oryx wa kilo 15 ulikuwa ukiuzwa kwa Sh. 25,000 kutoka Sh. 20,000 iliyokuwa kwa miezi minne nyuma kabla ya wakati huo.

Sambamba na mtungi huo mdogo, ilielezwa kuwa mtungi wa kilo 30 ulipanda kutoka Sh. 45,000 hadi Sh. 58,000 kwa Dar es Salaam huku kwa mkoa wa Njombe ikipanda kutoka Sh. 52,000 hadi 58,000.

Aidha, ripoti hiyo ilionyesha kwamba miongoni mwa watu waliohojiwa na waandishi wetu walibainisha kuwa kutokana na kupanda kwa bidhaa hiyo, hawatakuwa na uwezo wa kumudu gharama za gesi na badala yake watarudi kutumia mkaa ambao kwa gunia unauzwa Sh. 27,000.

Kutokana na ripoti hiyo, yako mambo kadhaa yamebainika kuwa yalikuwa na kasoro, mojawapo ikiwamo saizi ya mitungi ikiwamo kilo 15 na 30 iliyoko sokoni chini ya kampuni zinazouza LPG ikiwamo Oryx Gas Tanzania Limited.

Baada ya taarifa hiyo kutoka, mamlaka husika pamoja na wadau katika biashara ya gesi, Orxy wakiwamo, zilitoa taarifa kuhusu usahihi wa bei hiyo katika soko na mitungi inayohusika.

Usahihi ni kwamba mitungi iliyoko sokoni ambayo kampuni ya Oryx na zinginezo zinauza ni ya kilo sita, kilo 15 na 38 badala ya kilo 15 (ulioelezwa kuwa ni mdogo) na kilo 30.

Bei za mitungi hiyo kwa wakati huo hadi sasa ni Sh. 24,000 kwa ule wa kilo sita na Sh. 58,000 wa kilo 15 wakati mtungi mkubwa kabisa wa kilo 38 unauzwa kwa Sh. 110,000 kutokana na bei elekezi ya mamlaka zinazosimamia nishati.

Kutokana na maelezo hayo, kuna uwezekano kwamba kuna mkanganyiko uliojitokeza miongoni mwa wadau, hivyo marekebisho na usahihi wa bei na saizi ya mitungi uliotolewa ndiyo sahihi. **MHARIRI**

HABARI KITAIFA

# IGP Sirro: 'Panya Road' wamenivunjia heshima

**Na Romana Mallya**

SIKU chache baada ya kundi la vijana wanaofanya uhalifu mitaani, maarufu panya road kuvamia nyumba 23 eneo la Chanika jijini Dar es Salaam kisha kujeruhi na kupora mali za raia, Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, amesema kitendo hicho ni sawa na kumvunjia heshima kwa kuwa uhalifu wa aina hiyo umefanyika anakoishi.

IGP Sirro alitoa kauli hiyo juzi Chanika wakati akiwa kwenye kikao ambacho kilihudhuriwa pia na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, walipotembelea majeruhi wa tukio hilo lililotokea usiku wa kuamkia Jumapili ya wiki iliyopita.

Akizungumza katika kikao hicho, IGP Sirro alisema Chanika ni kwake na ana miaka 28 anaishi huko na aliposikia habari ya tukio hilo la wananchi kuvamia na kujeruhiwa, alipata tabu.

"Lakini, ninajua historia ya Chanika, ndiyo maana kama mnakumbuka nilikazana tujenge Kituo cha Chanika, ndiyo maana kama mnakumbuka nilisema tuifanye kuwa Wilaya ya Kipolisi kwa sababu ninajua tabu ya vijana wetu.

"Niwape pole kwa kilichotokea lakini mimi siyo msemaji, niwahakikishie mahali anakotoka IGP kuwa na uhalifu wa namna hii ni kumdhalilisha IGP, narudia mahali anakotoka IGP kufanya matukio ya ovyo namna hii ni kumdhalilisha IGP."

Alisema Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na waziri wana mambo mengi ya kufanya, hivyo hawapaswi kuwapa shida ya kufikiria Chanika.

Aliwawaeleza wana Chanika kuwa vijana waliofanya hivyo watawapata na mali zilizochukuliwa zitapatikana.

"Bahati nzuri niliwahoji baadhi yao. Kwa mfano, Yunusi anachoeleza ni utoto ni kijana ana miaka 13 au 14 ni kijana wa kwetu, walichofanya wanakutana kwenye mchezo wa pool table, viwanja vya mpira wanavuta bangi, wanakunywa konyagi halafu wanakwenda kufanya kazi hii.

"Vijana wetu 10 wa Chanika walishiriki katika hili, vijana kutoka Mbagala, mjini Kariakoo takribani 21, jumla walikuwa 31, mali yetu imechukuliwa nyingi imepelekwa sehemu ambazo siwezi kusema, lakini tumepata mahali pa kuanzia, tutapata majibu," alifafanua.

IGP Sirro aliwaeleza wana Chanika kuwa anapoweka mguu mahali mara zote husimamia suala la haki.

"Huwezi kutafuta televisheni yako halafu anakuja mtu kufanya mambo ya ovyo ovyo, hii kwetu ni matatizo na ni fursa, Mheshimiwa Waziri nikueleze shida moja waliyonayo wana Chanika, baadhi yetu suala ni ubinafsi, bahati nzuri umelizungumzia hili nimekuwa nikipiga sana kelele," alisema.

Alibainisha kuwa askari waliopelekwa huko ni wachache kulinganishwa na idadi ya wananchi na ili kuziba pengo hilo ni suala la kuwa na vikundi vya ulinzi shirikishi.

"Lakini, Mheshimiwa Waziri mtu ana kuambia 'Mimi nina kitu gani? Nitakuja kuibiwa kitu gani?' Akiwa na nyumba yake akiwa na chumba chake ukimwambia changia Sh. 1,000 anasema 'wachangie matajiri' sasa ndugu zangu kama mtaa hakuna mtu usiku, hakuna ulinzi shirikishi, mtaa utakuwa na vibaka tu.

"Huwa ninawaambia ukienda maeneo mengine kuna vikundi shirikishi, sasa wametoka Mbagala wamekuja kutuumiza kwa sababu hatuna ulinzi shirikishi, lakini sheria zipo ndogondogo, nilikuwa ninamuuliza Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, (Jumanne Muliro) tuchukue sheria zile tuwashtaki wasiotaka kushiriki ulinzi wa umma, ulinzi wa umma ni wa lazima.

"Mwingine anasema 'nina geti nina ulinzi wangu' hao watu 31 au 40 habari ya geti siyo kitu, wataingia watakushughulikia utakufa utaacha mali," alionya.

Masauni aliwasilisha pole za Rais Samia kwa wananchi hao na kuwaeleza kuwa lilimgusa, kumsononesha na kumsikitisha, hivyo akapewa maelekezo.

Katika mkutano huo mama mmoja ambaye watoto wake watatu walijeruhiwa baada ya kuvamiwa nyumbani kwake na kundi hilo aliishia kulia huku akimweleza waziri kuwa watoto wake wamepata matibabu lakini anadaiwa fedha za matibabu na uwezo hana.

# Wachumi watoa angalizo kupanda bei ya mafuta

**Na Waandishi Wetu**

WATAALAMU wa uchumi nchini wametoa angalizo kuhusu kupanda kwa bei za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa, wakitahadharisha kuwa kutasababisha kupanda kwa gharama za maisha.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Tanzania (EWURA) juzi ilitangaza bei kikomo ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kwa mwezi huu kukiwa na ongezeko.

Kwa mujibu wa tangazo hilo bei za mafuta ya petroli katika Jiji la Dar es Salaam ni Sh. 3,148 na dizeli Sh. 3,264 kwa lita. Tanga petroli itakuwa Sh. 3,161 wakati dizeli itakuwa Sh. 3,264 huku Mtwara petroli itauzwa kwa Sh. 3,177 na dizeli Sh. 3,309 kwa lita.

Mchumi na Profesa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Razack Lokina, aliiambia Nipashe jana kuwa mafuta yanapopanda bei yanaathiri sekta zote za kiuchumi hasa kupitia gharama za usafirishaji na uchukuzi.

Alisema hali hiyo itaathiri maisha ya watu kwa namna moja au nyingine kwa sababu nao ndiyo wahusika wakuu katika sekta hizo ikiwamo biashara, ajira na kilimo.

"Kwa hiyo, gharama za uzalishaji lazima zitaongezeka na kuwa na athari kwa ajira na biashara, ni wazi zitakuwapo na ni jambo la kawaida mfanyabiashara akishazoea bei kubwa mara nyingi hapendi kushusha hasa pale panapokuwa hakuna ushindani mkubwa kwenye biashara," alifafanua.

Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Donard Mmari, alisema kuna uwezekano mkubwa wa mfumuko wa bei kuongezeka, hivyo kupunguza thamani ya vipato halisi vya watu.

Alisema hali hiyo itasababisha watu kupunguza matumizi ya bidhaa na huduma mbalimbali, hasa zisizo za lazima, hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mchumi huyo alisema serikali inaweza kupunguza kidogo baadhi ya tozo katika bajeti ijayo ili kupunguza kasi ya kupanda bei ya mafuta.

"Pia inaweza kupunguza kidogo kodi ya mapato kwa kupanua wigo wa kodi ili kukuza pato halisi la watu. Pia kuongeza kasi ya kuvutia wawekezaji ili kuongeza uzalishaji wa baadhi ya bidhaa tunazoagiza nje kwa kutumia rasilimali zilizopo," alisema.

Mchumi Prof. Samwel Wangwe alisema kupanda kwa bei ya mafuta kunaweza kusababisha kupanda kwa bei za vitu vingine ili kufidia gharama zilizoongezeka.

Prof. Wangwe alishauri kupunguzwa kwa kodi zinazohusiana na mafuta ili kupunguza makali ya kupanda kwa bei ya nishati hiyo kwa wananchi ambazo pia zitasaidia kutopanda kwa bidhaa nyingine zinazohusiana na sekta ya usafiri.

MAPENDEKEZO ACT

Kutokana na hali hiyo, Chama cha ACT-Wazalendo kuja na hoja nne za kukabiliana na kasi hiyo ya ongezeko la bei za mafuta, kisisitiza hatua za haraka na za makusudi zinapaswa kuchukuliwa ili kuwanusuru wananchi kumudu gharama za maisha, zikiwamo nauli za mabasi na daladala zilizopandishwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Sekta ya Nishati wa ACT-Wazalendo, Is'haka Mchinjita, inapendekezwa serikali isimamishe kwa muda angalau Sh. 500 ya tozo katika kila lita ya petroli, dizeli na mafuta ya taa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kukabiliana na kupaa kwa bei ya mafuta, huku akieleza kuwa hatua hiyo wanatambua kwamba itaathiri bajeti ya serikali kwa wastani wa Sh. bilioni 200 kwa mwezi.

Aidha, alisema serikali isitishe kwa muda ununuzi wa ndege na ibane matumizi ili kufidia kodi hiyo itakapoondolewa.

Pendekezo la pili, ACT inashauri kutumiwa kwa fedha za akiba zilizoko kwenye mfuko wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kufidia kodi iliyoondolewa kwenye kodi ya petroli, dizeli na mafuta ya taa.

"Pendekezo la tatu, serikali iongeze uwezo wa kuagiza mafuta ili kuwa na akiba, kwa kuwa ni wazi kuwa kutokuwa na utamaduni wa kuwa na akiba ya mafuta ni miongoni mwa mambo yanayosababisha bei ya mafuta kupanda kila mwezi," alisema.

Aliongeza kuwa wakati wa serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kujenga utamaduni wa kuwa na akiba ya kutosha kwa angalau miezi sita ili kukabili dharura ya namna hii.

Pendekezo la nne, chama hicho kinashauri kuwekeza katika nishati mbadala ili kulinda uhuru, kuleta unafuu wa bei na nishati endelevu, huku akisema kuwa mpango wa kutumia gesi kama nishati mbadala umechelewa kuliko matarajio ambayo wananchi walipewa.

Pia alishauri kwamba kutokana na hali iliyopo nchini kwa sasa, ni muhimu kufikiria namna ya kutumia rasilimali za nchi kujikwamua kutoka kwenye majanga ya kinishati ambayo hawawezi kuyakabili moja kwa moja kwa kuwa hawayazalishi wenyewe.

Vile vile, ACT inatoa wito kwa serikali kuharakisha mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika, kwa kuweka wazi na kuwashirikisha wananchi juu ya mazungumzo, makubaliano na mikataba ya mradi huo.

"ACT-Wazalendo inaitaka serikali ichukue wajibu wake kwa wananchi na kuhakikisha kuna kuwa na ustawi wa wananchi," alisema.



# Mbunge Tarimba: Nikibahatika kuteta na Rais Samia nina haya kumweleza

## ■Asema uzoefu umemfungulia mengi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Kinondoni, Abbas Tarimba, ametaja mambo mawili yanayotawala kifikra zake, hata atakapopata faragha na Rais, atayawasilisha rasmi, akiyataja ni; kuwapo bima ya afya kwa kila Mtanzania, na maboresho kwa baadhi ya kodi.

Tarimba aliiambia Nipashe jijini hapa hivi karibuni kwamba ushuhuda wake wa magumu ya matibabu yanayoukabili umma, pia kasi ya kupanda kwa gharama za maisha kunaweka ulazima wa kuwapo hatua hizo, kuwaletea unafuu wananchi.

Mwanasiasa huyo ambaye awali alikuwa diwani, pia sasa anaongoza taasisi ya SportPesa, alisema mtazamo wake unatokana na alichokishuhudia muda wote kwenye uongozi wa kisiasa, pia watu wanavyoathiriwa na ongezeko la bei ya mahitaji muhimu linalojitokeza kwa sasa.

Ifuatayo ni sehemu ya mazungumzo ya Nipashe na mbunge huyo ambaye ni mdau mkubwa wa michezo:

**SWALI: Ukipata nafasi ya kuteta na Rais Samia japo kwa dakika moja, utamshauri jambo gani kubwa kwa Taifa?**

**TARIMBA:** Kwa upande wa kitaifa ninatamani sana tunakuwa na bima ya afya kwa kila Mtanzania. Nilipokuwa diwani na sasa mbunge, nimeona Watanzania wengi wanahangaika katika masuala ya afya kwenda kupata matibabu.

Hivyo, nikipata nafasi ya kuzungumza naye, nitamwambia Mheshimiwa Rais kwamba serikali ijipige kadri inavyoweza iweze kupata bima ya afya kwa kila Mtanzania.

La pili; nitamshauri kufanya mapitio ya kodi zote zinazomgusa mwananchi moja kwa moja ili kuzuia kupanda gharama za maisha.

Zipo kodi zinaweza kuangaliwa ili mwananchi wa kawaida aweze kupata nafuu ya kimaisha, hii inaweza kwenda sambamba na kutanua wigo wa watu kulipa kodi.

**SWALI: Kero kubwa ya Kinondoni kwa sasa ni ipi? Hatua zipi zimechukuliwa kuitatua?**

**TARIMBA:** Nilipoingia bungeni kwa mara ya kwanza mwaka 2020, mchango wangu wa kwanza ulikuwa ni kuiomba serikali kuharakisha kuanza kwa mradi wa Mto Msimbazi ili wananchi wanaopitiwa na mto huo waweze kuepukana na mafuriko ya mara kwa mara.

Kwa hiyo, moja ya ajenda yangu kubwa ni kuhakikisha tunapambana na hili tatizo la mafuriko. Ajenda yangu ya kwanza ikawa kuiomba serikali juu ya mradi wa Mto Msimbazi uweze kuanza. Na huo ndiyo ulikuwa mchango wangu wa kwanza kabisa nilipoingia bungeni. Bahati nzuri huo mradi unakwenda kuanza Julai mwaka huu na matatizo ya wakazi wa maeneo wanaopitiwa na Mto Msimbazi yanakwenda kuisha.

**SWALI: Ni mafaniko gani yamepatikana kwa muda mfupi ndani ya Jimbo la Kinondoni?**

**TARIMBA:** Mimi ni mkazi wa Kinondoni pia nimefanya uwekezaji hapo, hivyo mimi ni mdau kama walivyo wakazi wengine, mimi ni mkereketwa kama walivyo wakereketwa wengine wa maendeleo Kinondoni.

Nilitaka ubunge ili nisaidie kutoa huduma ambayo mimi mwenyewe ningependa kuipata kutoka kwa mbunge. Kuna vitu ambavyo tulikuwa tunakosa wakazi wa Kinondoni kwa muda mrefu.

Kinondoni ni jimbo lililoko mjini lakini lina changamoto nyingi. Karibia asilimia 75 ya eneo lake lipo kwenye mabonde na mito, hivyo wananchi wake wanapata matatizo makubwa wakati wa mvua.

Mimi nimewahi kuwa diwani kwa miaka 10, nimeona yanayotokea Kijitonyama, Makumbusho, Tandale, Mzimuni, Kigogo. Hivyo, moja ya ajenda yangu kubwa ni kuhakikisha tunapambana na hili tatizo la mafuriko.

Ajenda yangu ya kwanza ilikuwa ni kuiomba serikali juu ya mradi wa Mto Msimbazi uanze. Na huo ndiyo ulikuwa mchango wangu wa kwanza kabisa nilipoingia bungeni kama nilivyodokeza hapo awali.

Ninahangaika kuhakikisha wale watakaopitiwa na mradi huo na nyumba zao kubomolewa wanapata stahiki zao mapema. Nimekuta mradi wa Mto Ng'ombe ambao unapita katika maeneo mengi serikali ilishaanza kuutekeleza kwa Sh. bilioni 32.



Mbunge wa Kinondoni, Abbas Tarimba

Nilipoingia nilikuta mradi huu unasuasua sana, nikaanza kuufanyia kazi kwa kuhakikisha mkandarasi anakuwa kazini. Wananchi walikuwa wanahangaikia kulipwa fidia, lakini baadaye serikali ilitoka Sh. bilioni 4.3, hivyo kwangu ni mafanikio makubwa kwa wananchi kulipwa fidia zao.

Mimi nimelenga maeneo makuu yanayowagusa watu. Pia nimejikita katika kata ambazo hazijawahi kupata huduma za afya wala shule.

Kwa mfano, Kata ya Kinondoni haijawahi kuwa na huduma hizo. Nilichokifanya siku ya kwanza niliwachukua madiwani wote wa jimbo langu nikaja nao bungeni, tukakutana na Waziri wa TAMISEMI.

Niliwaleta ili waje waone mchakato pamoja na wao waongeze uzito. Hivi ninavyozungumza shule ya sekondari inajengwa katika Kata ya Kinondoni.

Sasa hivi pia kuna ujenzi wa kituo cha afya, hivyo katika kata zangu zote ambazo hazikuwa na huduma hizo zinakwenda kupata.

Kwenye Kituo cha Afya Kigogo tunahangaikia kupata fedha kwa ajili ya kujenga jengo la kuhifadhi maiti, tathmini imeshafanyika. Hivyo, kwenye maeneo ya kijamii tumefika mbali sana.

**SWALI: Unawezaje kujigawa kufanya majukumu ya kibunge, Mkurugenzi wa SportPesa na baba wa familia?**

**TARIMBA:** Ubunge kwangu mimi kama ibada, nikimwangalia binadamu ninauona utukufu wa Mungu, ninaona kumtumikia Mungu kupitia kuwatumikia binadamu.

Ukifanya kazi ya kumtumikia binadamu, wewe mwenyewe unanufaika. Mimi ninanufaika kwa imani yangu kupata rehema za Mungu.

Kuhusu SportPesa, nina wafanyakazi, siku hizi tunaendesha shughuli kwa mtandao, mafaili yote ninayaona kwa simu, ninapata muda wa kuyapitia, nikipata nafasi mwishoni mwa wiki ninakwenda ofisini.

Kwenye ubunge sijaharibikiwa, nikiwa hapa bungeni ninafanya shughuli zangu, mimi ni mjumbe wa kamati, ninafanya shughuli zangu vizuri. Ninapata nafasi ya kwenda jimboni kama kuna ziara au shughuli inayonihitaji ninakwenda.

Ubunge wangu ni wito, siuchukulii kama ajira, ninauchukulia kama wito wa kuwatumikia wanadamu pamoja na Tanzania.

Kuhusu familia, sina tatizo sana kwa sababu mke wangu anasimamia mambo yangu, biashara zangu, familia anasimamia yeye.

HABARI KITAIFA

# Serikali yaahidi ushirikiano kwa wawekezaji wapya

Na Benny Mwaipaja

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amewahakikishia wawekezaji kutoka Uingereza na Norway kwamba serikali itatoa ushirikiano mkubwa ili kufanikisha azma yao nchini kwa kuweka mazingira bora na vivutio kadhaa.

Dk. Nchemba alitoa ahadi hiyo jana jijini Dar es Salaam alipokutana na kufanya mazungumzo na kundi la wawekezaji kutoka Uingereza na Norway, wanaotaka kuwekeza katika sekta mbalimbali nchini.

Ujio wa wawekezaji hao wanaotaka kuwekeza kwenye sekta za kilimo, nishati, uchimbaji na uchakataji madini, ujenzi wa miundombinu mbalimbali, ni matunda ya ziara ya Samia Suluhu Hassan, aliyoifanya Ubelgiji na nchi za Kiarabu hivi karibuni.

Dk. Nchemba aliwahakikishia wawekezaji hao kwamba serikali itaendelea kuboresha sera za uwekezaji na kuwatoa hofu kwamba serikali ina sera za uwekezaji za uhakika, za kuvutia na zinazotabirika ili ushiriki kikamilifu katika biashara za kimataifa, kikanda na kukidhi soko la ndani.

Alisema amani na usalama vilivyopo nchini, upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kuwekeza, uwapo wa idadi kubwa ya watumiaji likiwamo soko la ndani na soko la ukanda, ni fursa nyingine itakayowawezesha wawekezaji hao kupata faida katika miradi yao.

Wakizungumza katika kikao hicho, wawekezaji hao walipongeza jitihada zinazochukuliwa na serikali ya Tanzania katika kuhamasisha uwekezaji pamoja na kuweka mazingira mazuri na rafiki ya uwekezaji na ufanyaji biashara.

Walisema wamekuja nchini kukutana na wadau zikiwamo wizara na taasisi mbalimbali ili kujifunza zaidi namna watakavyowekeza mitaji na teknolojia kwenye sekta za kilimo, uzalishaji wa umeme, uchakataji madini, mafuta na gesi.

Mwenyekiti wa wawekezaji hao, Lanre Akinola, alisema katika miaka michache ijayo, Tanzania inatabiriwa kuwa na uchumi imara na wenye nguvu zaidi kutokana na kutarajia kupata wawekezaji wengi kutoka Uingereza na Norway, hatua itakayokuza uchumi na kuzalisha ajira kwa wananchi.



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Kivule, jijini Dar es Salaam, Thobias Nyamboto, akipanda mti katika hospitali hiyo, uliotolewa na shirika linaloratibu mafunzo na uwezeshaji wa jamii kiuchumi na kimazingira la Equip For Change ambapo taasisi hiyo imepanda miti zaidi ya 1,500 hospitalini hapo. Anayeshuhudia ni Mkurugenzi wa Shirika hilo, John Wambura. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kifusi kilivyoua watoto na kujeruhi mama yao

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATOTO wawili wa familia moja, wakazi wa Kijiji cha Ngerengere, Kata ya Regicheri, Tarafa ya Inchugu wilayani Tarime mkoani Mara wamefariki dunia baada ya kufunikwa na kifusi wakati wakichimba kokoto kwa ajili ya biashara huku mama yao mzazi, Ghati Mrimi (30) akijeruhiwa. Watoto waliopoteza maisha ni Frank Mrimi (7) na mdogo wake Enjoy Mrimi (3). Mama yao alipelekwa Hospitali ya Stephen kwa ajili ya matibabu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana hospitalini huko mama huyo alisema: "Ninakumbuka ilikuwa Mei 2, mwaka huu majira ya 12 jioni, niliongozana na watoto wangu wawili; Frank anayesoma darasa la pili Shule ya Msingi Ng'ereng'ere na mdogo wake Enjoy, kwenda kuchimba kokoto kwa ajili ya kujipatia fedha za matumizi nyumbani.

"Tulipofika huko kwenye eneo linalochimbwa kokoto nilianza kuchimba kokoto huku watoto wangu hawa wakiwa wamekaa pembeni. Kwa bahati mbaya nilisikia kishindo kikubwa cha kifusi cha udongo kikitufunika mimi na watoto wangu hao.

"Nilijaribu kupiga kelele za kuomba msaada na watu waliokuwa karibu wakichimba kokoto na kufika na kutuondoa ndani ya kifusi, watoto wangu wote wawili Frank na Enjoy walikuwa wamefunikwa kabisa ilibidi wachimbe kufukua kifusi na kuwaondoa wakiwa hoi, nami nilikuwa katika hali mbaya, leo hii ninaweza hata kuongea, niliumia ubavuni na kichwani, watoto wangu sijui waliko," mama huyo asimulia akiwa hana taarifa kuhusu kuwapoteza watoto wake hao.

Mganga wa Hospitali hiyo, Dk. Stephen Mtimba, alisema kuwa majeruhi Ghati alifikishwa hospitalini huko Mei 2 mwaka huu akiwa katika hali mbaya kutokana na majeraha kichwani na ubavuni. "Alikuwa analalamika kuwa na maumivu makali, tulimpokea na kuanza kumpa huduma. Watoto wake wawili waliletwa hapa tukawapima, tukabaini walikuwa wamefariki (dunia) baada ya kufunikwa na kifusi na miili ya watoto hao ilipelekwa kuhifadhiwa katika chumba cha maiti Kituo cha Afya Sirari.

"Hatukutaka kumweleza huyu mama kuhusu watoto wake hao kuwa wamefariki (dunia), angejiongezea mawazo zaidi, kwa sasa hali yake inaendelea vizuri na huenda akaruhusiwa kwenda nyumbani leo (jana)," alisema Dk. Mtimba. Mwenyekiti wa Kijiji cha Ng'ereng'ere, Chacha Maseke na Diwani wa Regicheri, John Mbusiro, walisema wamesikitishwa na tukio hilo, wakitoa angalizo kwa wachimbaji wa kokoto kufuata utaratibu, ikiwamo kutokwenda na watoto kwenye shughuli za aina hiyo.

Kamanda wa Polisi Tarime/ Rorya, William Mkonda, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, akisema: "Jeshi la Polisi linawaonya wazazi na watu wanaokwenda kuchimba kokoto bila vibali na kutofuata Sheria za Utunzaji Mazingira za NEMC na kusababisha madhara, hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watu hao. Familia na Taifa limepata hasara kwa kuwapoteza watoto hao wawili."

# Askofu Moravian afariki dunia ghafla

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU wa Kanisa la Moravian Tanzania (KMT) Jimbo la Ziwa Tanganyika, Charles Katale amefariki dunia.

Taarifa iliyotolewa na Askofu Kiongozi wa KMT, Conrad Sikombe, ilisema Askofu Katale alifariki ghafla Mei 2, mwaka huu, baada ya kuugua muda mfupi.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Askofu Katale alifariki dunia wakati uongozi wa jimbo lenye makao makuu Kigoma, ukiwa katika mipango ya kumsafirisha kwa ndege kwenda Dar es Salaam kwa matibabu.

Kiongozi huyo amefariki dunia akiwa ametumikia wadhifa huo na kuwa askofu wa kwanza wa jimbo hilo, kwa takriban mwaka mmoja na miezi minne tangu alipoingizwa kazini Januari 10, mwaka jana, Urambo mkoani Tabora.

Kabla ya kuchaguliwa na kusimikwa katika wadhifa huo, Askofu Katale alikuwa Mwenyekiti wa Jimbo la Ziwa Tanganyika kwa miaka kadhaa. "Kutokana na msiba huu, tuendelee kuiombea familia yake, kanisa na jimbo alilokuwa akiliongoza," ilisema taarifa hiyo. Aidha, Askofu Kiongozi Sikombe katika taarifa hiyo, alisema Askofu Katale atakumbukwa kama mtu jasiri, mfundishaji mzuri na mhubiri wa injili mwenye karama.

Kuhusu mazishi ya askofu huyo, Katibu Mkuu wa KMT, Mchungaji David Mgombele, alisema maandalizi bado yanaendelea huku akibainisha kuwa viongozi wa kanisa hilo kutoka majimbo mbalimbali wako safarini kwenda Kigoma.

Hata hivyo, alisema ratiba ya awali inaonyesha kwamba mwili wa Askofu Katale utaagwa kesho na kuzikwa Jumamosi mjini Kigoma.

"Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina la Bwana lihimidiwe," ilimalizia taarifa hiyo.


## NAFASI YA KAZI

KAMPUNI INAYOONGOZA KWA UZALISHAJI WA CHUMVI TANZANIA INAKARIBISHA MAOMBI YA KAZI KUTOKA KWA WATU WENYE SIFA KWA NAFASI IFUATAYO.

**MENEJA MAUZO**
**NAFASI INAZINGATIA MAMBO MUHIMU YAFUATAYO :**
- KUENDELEZA NA KUONGEZA MAUZO YA KAMPUNI
- KUFIKIA MATARAJIO NA MALENGO YALIYOWEKWA
- KUANZISHA,KUIMARISHA NA KUPANUA WIGO WA WATEJA
- KUHUDUMIA MAHITAJI YA WATEJA WALIOPO
- KUONGEZA FURSA ZA BIASHARA KWA KUPITIA NJIA MBALIMBALI ZA MASOKO
- KUENDELEZA MIKAKATI YA MAUZO NA KUWEKA MALENGO
- KUKUSANYA NA KUCHANGANUA HESABU ZA MAUZO
- KUSHUGHULIKIA ANKARA ZA WATEJA WAKUBWA
- KUKUSANYA MAONI YA WATEJA NA UTAFITI WA MASOKO
- ATAWAJIBIKA KWA MAMENEJA WA JUU YAKE
- AENDANE NA WAKATI KUHUSU MAUZO NA WASHINDANI

**SIFA:**
- SHAHADA YA UTAWALA KATIKA BIASHARA [MASOKO]
- AWE NA UZOEFU WA MIAKA MITANO [5] KATIKA NAFASI HIYO
- AWE NA UZOEFU KATIKA KUPANGA NA KUTEKELEZA MIKAKATI YA MAUZO

**MAHALI PA KAZI: UVINZA, KIGOMA**

**MSHAHARA;** MSHAHARA NI MZURI KUTEGEMEA SIFA NA UZOEFU.

**MAOMBI YATUMWE KWA; nyanzasalt@gmail.com**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila mmoja atimize wajibu kuifanikisha sensa Agosti

**MAANDALIZI** ya Sensa ya Watu na Makazi itakayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu, yamefikia zaidi ya asilimia 81, na inakisiwa kwamba hadi kufikia Juni yatakuwa yamefikia asilimia 100.

Takwimu hizi ni kwa mujibu wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Sensa ya Watu na Makazi wakati akizungumza kwenye sherehe ya Siku ya Wafanyakazi Duniani jijini Dodoma. Majaliwa anawataka wafanyakazi kuwa mabalozi wa kuhamasisha ushiriki wa Watanzania katika Sensa ya Watu na Makazi lengo likiwa ni kuhakikisha kila Mtanzania anahesabiwa utakapofika wakati mwafaka.

Mwaka huu Taifa letu litakuwa linatekeleza shughuli hii kubwa na muhimu kwa maendeleo yake na wananchi kwa ujumla. Tunasema hivi kutokana na umuhimu wa sensa kwa maendeleo ya nchi.

Kwa sasa wimbo unaoimbwa na viongozi wa serikali na hata wa madhehebu ya dini ni kuhimiza Watanzania, ili wajiandae kwa wingi kuhesabiwa, kutokana na ukweli kwamba sensa ina umuhimu mkubwa na wa kipekee kwa maendeleo ya taifa.

Wakati wa maadhimisho ya Pasaka mwezi uliopita tuliwaona na kusikia viongozi wa Kikristo katika mahubiri yao kwenye ibada wakitoa msisitizo kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika sensa ili wahesabiwe, hivyo kuiwezesha serikali kuwa na takwimu sahihi kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo. Mufti wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubeir, juzi wakati wa swala ya Idd aliwataka waumini wa dini ya Kiislamu kujitokeza kushiriki katika sensa hiyo, kwa kuwa hilo ni jambo la wote na wasifuate kauli au yanayosemwa katika Uislamu hakuna sensa. Anahimiza Waislam na Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki suala hilo kwa kuwa ni haki kwa Waislamu na Watanzania kushiriki na kukubali kuhesabiwa kwa manufaa ya Taifa. Tunaamini sensa ni ya muhimu kwa ajili ya maendeleo ya taifa na watu kwa kuwa inasaidia serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Kimsingi, kuna masuala ya huduma za kijamii kuanzia kwenye afya, elimu na mengine muhimu ambayo serikali hainabudi kuyapata kupitia sensa, hivyo tunadhani ni vyema watu kuhesabiwa ili takwimu sahihi zipatikane. Bila kuwapo kwa takwimu sahihi, serikali inaweza kupata ugumu katika kupanga mipango yake itakayowezesha Watanzania kujiletea maendeleo, hivyo tunashauri kila Mtanzania ajiandae kuhesabiwa.

Lakini pamoja na hayo, tunashauri wale ambao watapewa jukumu la kuhesabu Watanzania, wafike kwa wakati kwenye maeneo husika, wawe na vitendea kazi vinavyotakiwa ili kupata takwimu kwa usahihi.


Hilo likifanyika, tunaamini kwamba, hakutakuwa na visingizio kutoka kwa wanaohesabiwa kwenda kwa makarani, kwamba hawakufika kwa wakati na kusababisha waondoke kwenye makazi yao kwenda kwenye shughuli zao. Wito wetu ni kwamba, makarani wafike kwa wakati wakiwa na vifaa vilivyokamilika, lakini siku hiyo watu wabaki nyumbani wahesabiwe kwanza ndipo waende katika shughuli zao na watoe taarifa sahihi kwa makarabi. Tunasisitiza kutoa taarifa sahihi, kwa sababu kumekuwapo na elimu potofu kuwa sensa inalenga kutambua watu waliopata chanjo ya UVIKO-19 na pia kuna dodosa linalohusiana na dini huku wapotoshaji pia wakidai kuwa serikali inawahesabu watu ili kuwadai kodi.

Hayo yalishatolewa ufafanuzi na serikali, lakini bado wale ambao hawajaelewa, tunawashauri wawe tayari kuhesabiwa na kutoa taarifa sahihi zitakazosaidia serikali kupanga shughuli za maendeleo kwa wananchi wake. Ikumbukwe kuwa, katika sensa kuna taarifa za msingi za kuwezesha serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi za mipango katika ngazi zote.

Kwa maana hiyo, kila upande utimize wajibu wake inavyotakiwa kuanzia wanaohesabu watu, wale wanaohesabiwa ili kile ambacho serikali imekusudia kukifanya kupitia sensa hiyo, kifanikiwe.

Tunaamini pia kuwa serikali kwa upande wake itahakikisha kwamba maandalizi hayo yatakuwa yamekamilika kwa asilimia 100 kabla ya kufanyika kwa sensa hiyo, ikiwamo kufanyika kwa sensa ya majaribio.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



### KILELE SIKU YA WAKUNGA LEO

# Maadhimisho yaje na mbinu mpya zaidi kunusuru wajawazito, watoto

Na Sabato Kasika

**KATIKA** kupambana na vifo vya wajawazito, serikali imechukua hatua mbalimbali, zikiwamo kuanzisha kampeni maalum ya 'Jiongeze Tuwavushe Salama' iliyoanzishwa na aliyekuwa Makamu wa Rais na sasa, Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Mbali na kampeni hiyo, serikali imejenga vituo vingi vya huduma za afya ngazi zote, ambayo wajawazito wanajitokeza kuhudhuria kliniki, ili kuhakikisha wanakuwa salama, tangu mimba hadi kujifungua.

Katika kuimarisha mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji taarifa za wajawazito, wameshaanza kuimarisha na kufuatilia maisha ya kila mmoja tangu anapopata ujauzito, muda wa kuanza kliniki, kujifungua hadi kuvusha siku 42 baada ya kujifungua.

Binafsi, ninaamini ni mfumo unaoweza kusaidia kuokoa maisha ya wajawazito nchini, kutokana na kupitia mfumo huo serikalini, inapata taarifa za wajawazito kujua ni aina gani ya dawa zinazohitajika kumhudumia mjamzito.

Kwa nini? Sababu kubwa ni kwamba, serikali inasema mfumo huo utaeleza uhalisi wa miundombinu iliyopo na unaohitajika, hali kadhalika uwajibikaji wa watumishi wa afya kwa ujumla wao, hata mmoja mmoja, ili kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wajawazito.

Ni wazi kwamba, njia hiyo inaweza kuwa na manufaa katika kupunguza vifo vitokanavyo uzazi kwani inalenga kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa kila mjamzito, ili kuokoa maisha yao na watoto wachanga.

Wakati leo ni kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani, huku wadau wa afya ya uzazi wakiwa na maoni yao wanayoamini kwamba yakifanyiwa kazi, yanaweza kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi nchini.

Miongoni mwa maoni hayo, ni serikali kuwekeza zaidi katika kuboresha mazingira ya kazi na ubora wa vitendea kazi kama njia mojawapo ya kukabiliana na vifo, hivyo vinavyogusa pia watoto wachanga.

Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA), kinasema licha ya kuwapo taarifa zinazotolewa na serikali na wadau mbalimbali, zikionyesha kuongezeka hospitali na vituo vya afya kitaifa, lakini viwango vya vifo vya uzazi bado vimeendelea kuwa juu.

Hata hivyo, inakiri na kutambua hatua kubwa ambazo Tanzania imeendelea kuzipiga, ili kupunguza vifo vya mama na mtoto wenyue umri chini ya miaka mitano, lakini inatamani juhudi zaidi zifanyike, nchi ifikie lengo la maendeleo endelevu la asilimia 70 kwa vizazi 100,000 na kuondoa vifo vinavyoweza kuepukika mwaka ifikapo mwaka 2030.

Hivyo basi, wakati dunia inaadhimisha Siku ya Wakunga Duniani, ninadhani ipo haja kwa ushauri huo ukafanyiwa kazi, ili kuendelea kuokoa maisha ya Watanzania wanaojifungua na hata watoto wachanga waliopo hadi wenye umri wa miaka mitano.

Suala la kuwekeza zaidi katika ukunga kama inavyoshauri TAMA, mara zote ni jambo muhimu, kwani wakunga wanahimiza wakiwa wengi, inawasaidia kupunguza vifo inavyotokana na uzazi.

Nakumbuka, Naibu Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Afya, Uzazi na Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, Dk. Wilfred Ochan, anahimiza Siku ya Wakunga Duniani, ina nafasi ya kuangalia takwimu na jinsi uwekezaji ulivyo kwenye ukunga nchini.

Anatilia mkazo, vifo vingi vinavyotokana na uzazi vinazuilika, hasa kukiwapo huduma bora kutoka kwa wataalamu waliowezesha, ili wasaidie kutoa huduma tangu hatua ya mimba hadi mtoto anapozaliwa.

Anakiri, ripoti ya UNFPA ya mwaka kuhusu Shirikisho la Wakunga na WHO, ina angalizo iwapo serikali duniani zitawekeza kwa wakunga, maisha ya watu mlioni 4.3 yanaweza kuokolewa kila mwaka kuanzia mwaka 2035.

Kwa maana hiyo, ni wazi kwamba uwekezaji zaidi unatakiwa kufanyika kwenye afya za wajawazito, ili kuhakikisha wanajifungua salama, pia watoto wanaozaliwa nao wanabaki salama.

## Mpango Barrick wapaisha ufaulu

Na Mwandishi Wetu

MPANGO wa kuinua ufaulu shuleni (Performance Improvement Program (PIP)) unaotekelezwa na kampuni ya Barrick kupitia mgodi wa Bulyanhulu, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Nyang'hwale mkoani Geita, umefanikiwa kupata matokeo mazuri kwa kuongeza idadi ya ufaulu wa wanafunzi wilayani humo.

Kabla ya kuanzishwa mpango huu unaolenga shule za sekondari, ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne wilayani humo kwa kiwango cha daraja la kwanza ulikuwa wa wanafunzi watano, lakini kwa sasa idadi imeongezeka kufikia wanafunzi 55.

Mafanikio hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya kuwatunukia zawadi wanafunzi kutoka shule mbalimbali waliofaulu vizuri sambamba na walimu waliofanikisha ufaulu huo kupitia programu ya PIP.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo iliyohudhuriwa na walimu, wazazi, wanafunzi na wafanyakazi wa Barrick alikuwa Mkuu wa wilaya hiyo, David Jamhuri.

Progamu hii ilianzishwa mwaka 2019 kwa lengo la kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa shule za sekondari na kupunguza utoro shuleni hususani kwa wasichana. Kutokana na matokeo chanya ya mpango huu kwa wanafunzi, Kamati ya Maendeleo ya Jamii (CDC) imekuwa ikitenga fedha kila mwaka ili kufanikisha utekelezwaji wake.

Meneja wa Mahusiano ya Kijamii wa Barrick Bulyanhulu, Agapiti Paul, alisema katika kipindi cha mwaka 2021 kampuni ilitenga Sh. milioni 50 kwenye bajeti ya miradi ya kijamii (CSR) katika Halmashauri ya Nyang'hwale, kwa ajili ya kununua vitabu kwa ajili ya wanafunzi na walimu katika shule 10 za sekondari za serikali wilayani humo, kutoa zawadi za motisha kwa wanafunzi waliofaulu kwa daraja la kwanza, wazazi wa wanafunzi hao, walimu ambao masomo wanayofundisha wanafunzi waliyafaulu vizuri na shule ambazo zimepata wanafunzi wenye ufaulu huo.

Jamhuri alipongeza jitihada zinazofanywa na Barrick kutoa motisha kwa walimu na wanafunzi kwa lengo la kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wilayani humo. "Naamini ushirikiano wa serikali na Barrick kupitia mpango huu utaleta mafanikio makubwa zaidi, natoa wito kwa walimu na wanafunzi kuongeza bidii wakati wote kufanikisha malengo ya serikali ya kuboresha sekta ya elimu ya elimu nchini ambayo inazidi kuboresha miundombinu shuleni na kukabili changamoto mbalimbali zilizopo," alisema.

Mmoja wa wanafunzi aliyenufaika na mpango huu, Egide John Halalawe kutoka Sekondari ya Msalala akizungumza kwa niaba ya wenzake, alisema kupitia mpango huo wanafunzi wananufaika kwa kupata vitabu pia kupatiwa chakula shuleni na umewezesha walimu kufundisha kwa bidii na kusimamia kwa karibu wanafunzi wanapokuwa kwenye mwaka wa mtihani.

"Tunashukuru Barrick na Halmashauri kwa kubuni mpango huu, tuna imani utawezesha wanafunzi wengi kufanya vizuri zaidi katika mitihani yao ikiwamo kupata daraja la kwanza na madaraja mengine ya juu ya ufaulu," alisema.

# ACT yatangaza kongamano la pili Tume Huru Uchaguzi

Na Mwandishi Wetu, MWANZA

UONGOZI wa Chama cha ACT- Wazalendo umesema chama hicho kinatarajiwa kufanya kongamano la pili la Tume Huru ya Uchaguzi kuelekea Katiba Mpya keshokutwa jijini Mwanza.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Janeth Rithe, Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma wa chama hicho, kongamano hilo limepangwa kufanyika keshokutwa kwenye Hoteli ya Aspen jijini humo. Katika taarifa yake hiyo, Janeth alibainisha kuwa leo ni maadhimisho ya kitaifa ya siku ya kuzaliwa kwa ACT- Wazalendo, chama hicho kikipata usajili wa kudumu Mei 5, 2014.

Janeth alisema maadhimisho ya kitaifa ya kuzaliwa kwa chama hicho yatafanyika jijini hapo leo, wanachama na viongozi wa chama wakitarajiwa kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo kuchangia damu, kuwajulia hali na kuwafariji wagonjwa, kupanda miti na kufanya usafi shuleni na hospitalini.

"Maadhimisho hayo yatahudhuriwa na viongozi wakuu wa kitaifa akiwamo Kiongozi wa Chama, Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Chama, Juma Duni Haji, Makamu Mwenyekiti Bara, Dorothy Semu na Katibu Mkuu, Ado Shaibu.

"Tarehe 06 Mei (kesho), viongozi hao sambamba na viongozi na wanachama wa Mkoa wa Mwanza watashiriki programu ya chama itakayohusisha uzinduzi wa ofisi za chama za mkoa, majimbo na ufunguzi wa matawi ya chama," Janeth alifafanua katika taarifa yake hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale, David Jamhuri (wapili kulia), akimkabidhi zawadi mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Msalala, Egide John Halalawe, katika hafla ya kukabidhi zawadi kwa walimu na wanafunzi waliofanikisha mpango wa kuinua ufaulu shuleni unaotekelezwa na Barrick Bulyanhulu kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya katika mikoa ya Shinyanga na Geita. Wengine pichani ni maofisa wa Barrick na viongozi wa serikali wilayani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Njombe awashukia wanaume wanaowapa mimba wanafunzi

Na Elizabeth John, NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba, amewaonya wanaume wanaowapa mimba wanafunzi kuwa sheria itawashughulikia.

Kindamba aliyasema hayo kwenye kikao cha wadau wa elimu kuwa kurudishwa shule wa wanafunzi waliopata mimba sio mwanya wa kuharibu ndoto za wasichana hao.

"Hii sio sababu ya kwenda kupachika mimba watoto wadogo wa shule, serikali ipo, sheria zipo, twendeni tukawashughulikie wanaosababisha utoro kwa wanafunzi kwa sababu ya mimba haikubaliki," alisema Kindamba.

"Na saa nyingine unakuta sisi mababa majitu mazima kabisa tunaacha watu wazima wenzetu tunakwenda kudandia watoto wa shule, kuna kipindi kulikuwa na kampeni nzuri sana ilikuwa inasema sidanganyiki. Twendeni na sisi tukatengeneze kampeni yetu nzuri kabisa hata kwa kuweka mabango shuleni inayosema wanafunzi wasidanganyike," alisema Kindamba.

Mkuu wa mkoa alisema kumpa mimba mwanafunzi ni kuharibu ndoto zake. "Sheria ni lazima zisimame, lakini ionekane inasimamiwa na ikitokea umefanya sheria kali itakushughulikia. Tutakuangukia kwa nguvu zetu zote ukishaenda ujumbe kwa watu wawili watatu umewashughulikia hao mabazazi wengine wenye tabia mbaya namna hiyo hawatofanya," alisema.

Pia, aliagiza Idara ya Elimu mkoa kuhakikisha wanafunzi wa shule ya sekondari 821 ambao hawajaripoti shuleni kwa ajili ya kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022 watafutwe popote walipo ili waeleze sababu za kutoripoti.

Awali, akitoa taarifa ya tathmini ya elimu, Ofisa Elimu Mkoa wa Njombe, Nelasi Mulungu, alisema wanafunzi zaidi ya 800 hawajaripoti katikashulewalizopangiwakwa ajili ya kidato cha kwanza 2022.

# Wanafunzi wajipanga kutoa elimu ya rushwa shuleni

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

KLABU ya Wapinga Rushwa katika Shule ya Sekondari Kibiti, imeeleza kuwa imejipanga kutoa elimu kwa kuanzisha midahalo ya wazi kuelimisha kuhusiana na mapambano ya rushwa na kuifikisha kwa watoto shuleni.

Hayo yameelezwa na wanafunzi wa klabu hiyo ambao wamesema watahakikisha kuanzia watoto wanapata elimu ya rushwa ili hata wanapokuwa wakubwa wanajenga tabia ya kuichukia.

Akielezea hayo juzi mmoja wa wanafunzi wa klabu ya kupinga rushwa ambayo ni muungano wa TAKUKURU na Skauti, Chai Kiseja, alisema wanatarajia kutumia mbinu mbalimbali ikiwamo ya sanaa kufikisha ujumbe.

Alisema kuwapo kwa rushwa kunachangia wananchi kukosa imani na serikali katika mambo mbalimbali, pia mmomonyoko wa maadili.

Rajab Said kutoka ofisi ya TAKUKURU Kibiti, alisema tayari wameanzisha klabu za kupinga rushwa katika shule 10 za wilaya hiyo ambazo ni muunganiko wa Skauti na TAKUKURU.

Alisema walibaini skauti kuwa na jeshi kubwa ambalo litasaidia kuongeza nguvu kwa kuungana na klabu hizo na kutoa elimu ya kupinga rushwa.



Viongozi wa Jumuiya za Wasimamizi wa Fukwe na Mazingira (BMU), kata ya Moa, wilayani Mkinga, mkoani Tanga, wakiwa kwenye mtumbwi kabla ya kuondoka kwenda kutembelea visiwa ikiwa ni sehemu ya ukaguzi wa fukwe za bahari, jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# TASAF yasaidia watoto kaya maskini vifaa vya shule

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji Njombe imepokea vifaa vya usafi kwa ajili ya watoto wa kike 1,501 katika shule za sekondari ambazo kaya zao zinanufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF), kila mtoto atapatiwa ndoo, taulo za kike, sabuni na nguo za ndani.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa hivyo iliyofanyika katika Kata ya Uwemba, Kijiji cha Uwemba, Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Mji Njombe, Peter Magehema, alisema vifaa hivyo vitasambazwa kwa kila mtoto ambaye kaya yake inanufaika na mpango huo katika kata zote 13.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Kuluthum Sadick, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, alishukuru UNICEF kwa hatua hiyo ambayo itasaidia watoto wa kike kusoma katika mazingira safi na salama.

Katika hatua nyingine Kuluthum aliwataka watoto hao kusoma kwa bidii bila kujali mazingira waliyotokea kwa kuwa elimu wanayoipata ni kwa ajili ya maisha yao na kuwaonya wasikubali kurubuniwa na kupoteza mwelekeo wao wa elimu.

"Nyie mpo shuleni kwa ajili ya kutafuta maisha yenu. Kama kuna vitu ambavyo mzazi wako anakupatia mfano mahitaji ya shuleni au kama mzazi wako hakupatii hayo ni maisha ya mzazi wako, tunawashukuru kwa kutuleta duniani na kutupatia yale yaliyo kwenye uwezo wao. Lakini nyie mpo kwa ajili ya kuyapambania maisha yenu, niwaombe msome kwa bidii ili mfaulu mitihani yenu," alisema Kuluthum.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa vifaa hivyo, mwanafunzi Efgenia Mwalongo, alisema wanashukuru kwa msaada huo kwa kuwa utawasaidia kuwa na mazingira salama na huru ya kusoma shuleni.

# Mabadiliko makubwa sekta elimu sasa yaja

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imetangaza kuleta mabadiliko makubwa katika Sekta ya Elimu nchini kuanzia Shule ya Msingi ikiwamo kuwaandaa wanafunzi kujifunza kwa vitendo elimu ya masomo ya kilimo na michepua ya Sayansi Kimu ili waweze kupata ujuzi wa kukidhi matakwa ya ajira ikiwamo kwenye Sekta ya Utalii.

Kupitia mpango huo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), wameshaweka mikakati ya kuwandaa walimu kwa kuwapa mafunzo ndani na nje ya nchi ili kuwafundisha wanafunzi.

Mkakati huo umetangazwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, wakati akifungua mafunzo maalumu kwa walimu 322 wa masomo ya Mchepuo wa Kilimo na Sayansi Kimu kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar yaliyofanyika Morogoro.

Prof. Mkenda alisema tayari wizara hiyo imeanza kutoa kipaumbele kwa mafunzo ya walimu wa masomo hayo nchini kwa kuwaongezea ujuzi na maarifa ya kwenda kuwafundisha wanafunzi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuandaa vijana ambao wataweza kuongeza ajira katika Sekta ya Kilimo na Utalii ambao tayari umeshatangazwa nje ya nchi na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia filamu ya utalii ya 'The Royal Tour'.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Aneth Komba, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa kitaalamu walimu wa masomo ya Sayansi Kimu na Kilimo kwa kuwapa mbinu za ufundishaji, ujifunzaji na upimaji unaozingatia ujenzi wa umahiri.

Dk. Komba alisema kuwa matokeo ya mafunzo hayo yatamwezesha mhitimu wa masomo hayo kupata maarifa, stadi za kutenda uelekeo wa kujitegemea kwa manufaa mapana ya jamii na taifa kwa ujumla.

Alisema mafunzo ni ya kundi la tatu la walimu 322 ambao wanatoka katika shule za serikali na binafsi ili kuwajengea uwezo mkubwa wanafunzi ambao wataingia katika soko la ajira.

Naye Kaimu Naibu Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Hadija Mcheka, alisema mafunzo hayo yamekuja kwa wakati kutokana na kuwapo kwa upungufu mkubwa wa walimu wa masomo hayo na kwamba wataendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu kusaidia kuongeza idadi ya walimu.

# Watakiwa kufuata utaratibu wa kazi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAFANYAKAZI wa taasisi za umma kisiwani Pemba wametakiwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kufuata utaratibu, huku wakiwa na utayari katika kufanya kazi zao za kila siku.

Hayo yalisemwa na Ofisa Mdhamini Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Pemba, Halima Khamis Ali, katika mafunzo ya Sheria nambari 2 ya mwaka 2011 na Kanuni za Utumishi wa Umma mwaka 2014 kwa wafanyakazi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

Akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika katika Ukumbi wa Nyaraka Chake Chake, Halima alisema iwapo watafanya kazi kwa kufuata utaratibu unaofaa, watakuwa watendaji wazuri wa kazi zao.

Alisema ni lazima kila mfanyakazi wa taasisi za umma kufuata utaratibu katika kazi na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa kanuni, sheria na miongozo ya utumishi.

"Mafunzo haya ni kwa ajili ya kutuongezea ufanisi katika kazi zetu, hivyo tuzijue sheria na kanuni za utumishi ili tuweze kufuata utaratibu unaotakiwa," alisema mdhamini huyo.

Mdhamini huyo aliongeza kuwa, ikiwa watumishi watafanyakazi kwa kutokujua wajibu wao wanaweza kukosa hata haki zao za msingi, hivyo wawajibike ipasavyo katika utendaji wa kazi zao.

Aidha, aliwataka wafanyakazi wa taasisi hizo kujiepusha na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi, kwani ni janga linalorudisha nyuma maendeleo ya nchi.

Ofisa Mdhamini Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Zuhura Mgeni Othman, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa wafanyakazi, kwa kuwa yataenda sambamba na ufanisi wa kazi zao.

"Ni imani yangu kwamba baada ya mafunzo haya mtabadilika na kuongeza kasi ya utendaji," alieleza mdhamini huyo.

Naye Rehema Alawi Abdalla kutoka Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi alisema, mtumishi yeyote anatakiwa kujua majukumu yake pamoja na kujaza viwango vya kupima utendaji kwa kushirikiana na mkuu wa kitengo.

Mwasilishaji kutoka Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Badria Salim Ali, alieleza utafiti unaonyesha kwenye taasisi za umma kuna uwezekano mkubwa wa kufanyika vitendo vya rushwa na ndio maana serikali ikaunda mamlaka maalumu ya kupambana.

"Rushwa imeenea katika jamii zetu na bado walio wengi hawana uelewa kwa sababu hudanganywa kwa kuambiwa watoe rushwa kwa ajili ya kupata ajira, zipo kesi hizo, kwa kweli jambo hili ni baya," alisema mwasilishaji huyo.

Alifahamisha kuwa, kutumia mali vibaya, kukwepa kulipa kodi, kufanya biashara ya magendo, kuficha bidhaa, kutumia vibaya taarifa za ofisi na usafishaji wa fedha haramu ni uhujumu wa uchumi ambao husababisha kuhujumu mali za serikali.

Washiriki wa mafunzo hayo waliiomba Wizara ya Utumishi kuwapelekea maofini mwao Sheria za Utumishi wa Umma ili wazisome mara kwa mara, jambo ambalo litasaidia kujua haki na wajibu wao katika kazi.

# Serikali yataka wenye ulemavu kukumbukwa

**Na Frank Monyo**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Jamal Katundu, ametoa wito kwa jamii kuwakumbuka na kuwajali watu wenye ulemavu kwani kundi hilo lina nafasi muhimu katika kuleta maendeleo ya Taifa.

Ametoa wito huo, aliposhiriki chakula cha mchana na jamii ya wanafunzi na watumishi wa Chuo cha Ufundi Stadi kwa watu wenye ulemavu Yombo cha jijini Dar es Salaam katika kusherehekea sikukuu ya Idd el Fitr.

"Nitoe wito kwa jamii kwa ujumla kutenga muda wao kwa ajili ya kujumuika na watu wenye ulemavu ili kuendelea kuwapa faraja na kuwatia moyo wa kuendelea kujituma na kutoa mchango wao katika ujenzi wa taifa letu kwa kadri inavyowezekana," alisema Prof. Katundu na kuongeza:

"Kwa upande wetu sisi kama serikali tunaendelea kutimiza wajibu wetu wa kuwahudumia Watanzania wote bila kujali hali zao na ndio maana leo tumeona ni vema kujumuika na vijana wetu wenye ulemavu ambao wanapatiwa mafunzo katika chuo hiki ambacho ni miongoni mwa vyuo vyetu vilivyopo katika kanda mbalimbali kwa ajili ya kuwalea na kuwapa ujuzi vijana wenye ulemavu wa aina tofauti ikiwamo uziwi, ulemavu wa ngozi, ulemavu wa viungo nakadhalika."

Katibu Mkuu huyo alisema serikali imeanza kufanya maboresho ya miundombinu katika vyuo vya ufundi vya watu wenye ulemavu nchini ili kuliwezesha kundi hilo maalum kupata ujuzi muhimu utakaoliwezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

"Nadhani, mmeshaliona lile gari kubwa ambalo limekuwa likija hapa chuoni, mnajua linaleta nini?" Aliwauliza wanafunzi wa chuo hicho ambao waliitikia, "maru maru."

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu, Prof. Jamal Katundu na Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Mariam Chelangwa, serikali imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu mbalimbali yakiwamo mabweni na vyumba vya madarasa katika chuo hicho na vingine vilivyoko Singida, Tabora, Mwanza, Tanga na Mtwara ambapo tayari baadhi ya vifaa vya ujenzi vimeshaanza kufikishwa katika vyuo husika.

Katika ziara hiyo, Katibu Mkuu huyo ameambatana na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda, ambaye alisema lengo la kuandaa na kushiriki chakula cha pamoja na jamii hiyo ya wanafunzi na watumishi wa chuo ni kuendelea kutoa faraja kwa kundi hilo muhimu katika jamii ambalo mara nyingi limekuwa likisahaulika.

"Tumekuja hapa kwasababu tunatambua kuwa watu wenye ulemavu ni sehemu ya jamii lakini kwa muda mrefu watoto hawa wanakuwa pekee yao pamoja na walezi wao tu hivyo wanatuhitaji sana kwa ajili ya kuendelea kuwatia moyo na kuwafariji.

Hivyo sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu tumeona leo tuje tujumuike nao kwa kula pamoja, kuongea na kucheza nao kama namna ya kuendelea kuwapa faraja na kuwahamasisha kuendelea kujibidiisha katika masomo yao.

Na si hivyo tu, kuja kwetu hapa kunatuwezesha kufahamu changamoto zao na kupata mrejesho zaidi wa maendeleo ya vyuo vyetu," alisema Mtendaji Mkuu wa OSHA.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Mariam Chelangwa na mmoja wa wakufunzi wa chuo hicho, Aloyce Nkuna, wamewashukuru viongozi waliowatembelea na serikali kwa ujumla kwa jitahada mbalimbali zinazochukuliwa katika kuwezesha chuo kuendelea kutekeleza wajibu wake kikamilifu.



Mbunge wa Ushetu mkoani Shinyanga, Emmanuel Cherehani (kushoto), akizungumza na wananchi wa kata ya Uyogo jana, wakati wa ziara yake ya kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Stendi ya daladala Mafiga kupandishwa hadhi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

BARAZA la Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro limemwagiza Mkurugenzi wake, Ally Machela, kuanzisha haraka mchakato wa kuifanya stendi ya daladala ya Mafiga ipandishwe hadhi kuwa ya Wilaya ya Morogoro ili itumiwe na magari yanayosafirisha abiria katika ya mkoa wa Morogoro.

Meya wa Manispaa hiyo, Pascal Kihanga, alitoa agizo hilo kwa niaba ya madiwani kwenye kikao cha kawaida cha baraza la madiwani kilichofanyika juzi katika soko kuu la Chifu Kingalu mjini Morogoro.

"Kati ya masuala tuliyoamua kubwa ni stendi ya Mafiga na kumwelekeza mkurugenzi aanze mchakato kwenda kuwa stendi ya wilaya badala ya kuwa ya daladala na mchakato huu uharakishwe," alisema Kihanga.

Alisema lengo lake ni pamoja mabasi yanayotoka ndani ya mkoa wa Morogoro yaishie stendi ya Mafiga, huku Stendi ya Mkoa ya Msamvu ibaki kwa mabasi yanayokwenda mikoani Ujenzi wa Stendi ya Daladala Mafiga hadi ulipokamilika uligharimu Sh. 5,243,115,225.55 ambapo lengo lilikuwa ni utasaidia kuondoa msongamano wa magari eneo la kati la mji unaosababishwa daladala eneo la stendi iliyokuwa ikitumiwa awali.

Mbali na kuondoa msongamano pia kuongeza fursa za kibiashara na kiuchumi kwa wakazi wa Manispaa, na kuongeza vyanzo vya mapato kwa halmashauri.

# Serikali ilivyojipanga kuwaongeza watalii

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI kupitia taasisi zake zilizoko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ikiwamo Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imejipanga katika maeneo kuhakikisha inawavutia watalii kuja kuwekeza nchini.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, katika ofisi ya makao makuu ya Tawa yaliyoko, Manispaa ya Morogoro ikiwa sehemu ya ziara yake ya kikazi na kuzungumza na watumishi ikiwa ni ziara yake ya kwanza tangu ateuliwe kushika wadhifa huo.

Alisema kutokana na mkakati huo, Chana alipongeza TAWA kwa kutenga maeneo ya uwekezaji katika mapori ya akiba na maeneo mengine inayoimiliki ili kuendelea kuwavutia watalii kutoka maeneo mbalimbali duniani.

Chana alisema uwekezaji mkubwa uliofanywa na mamlaka hiyo kwa sasa utaleta matunda mazuri kufuatia kutokana na filamu ya Royal Tour.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni alizindua filamu ya Royal Tour katika majiji ya New York na Los Angeles nchini Marekani, filamu ambayo inaonyesha vivutio mbalimbali vilivyoko Tanzania na hivyo itasaidia kuongeza idadi ya watalii nchini mara mbili zaidi ya sasa.

Waziri Chana aliiagiza menejimenti na watumishi wa mamlaka hiyo kuwa tayari kujipanga na kupokea wageni watakaokuja nchini yakiwa ni matokeo ya filamu ya Royal Tour, huku akiipongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhifadhi rasilimali za maliasili kote nchini.

Aliwataka wawekezaji wa kutoka nje ya nchi na wa ndani ya nchi kutumia fursa kuwekeza katika utalii kwani milango ipo wazi.

Alisema utalii unachangia asilimia 17 ya pato la Taifa na pia unasaidia kuongeza ajira kwa Watanzania hivyo Royal Tour inakumbusha taratibu kwa wageni wanapokuja kufanyika kwa haraka.

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, Mabula Misungwi Nyanda, alisema mamlaka imepata mafanikio mbalimbali ikiwamo kupungua kwa shughuli za ujangili.

Alitaja mengine ni kuimarika kwa shughuli za uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori, ugawaji wa vitalu vya uwindaji kwa njia ya mnada wa kielektroniki na uboreshaji wa miundombinu ya utalii kwenye maeneo ya hifadhi.

Alitaja maeneo baadhi ya maeneo ambayo wamejipanga kupokea watalii mbalimbali kutoka sehemu tofauti duniani na kutembelea vivutio vinavyosimamiwa na mamlaka hiyo yakiwamo mapori ya akiba ya Pande, Mpanga Kipengere, Mkungunero, Kijershi na Swangaswanga.

Mengine ni ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara ambayo ni malikale yaliyomo katika orodha ya urithi wa utamaduni wa dunia na yanasimamiwa chini ya mkataba wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ambayo wanawavutia watalii wengi duniani.




Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Dodoma, Ahidi Sinene, akipanda mti wakati wa zoezi la kupanda miti 2,000 katika eneo la Hospitali ya Mirembe, jijini Dodoma jana. Waliosimama ni baadhi ya washiriki wa kampeni ya upandaji miti. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Wazee Kilimanjaro waguswa msaada wa SBL

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya wazee wanaoishi Mwika mkoani Kilimanjaro wameitaka jamii kuliangalia kundi hilo ambalo limetumia nguvu kubwa kulitumikia taifa huku wakitoa shukrani kwa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kwa kutoa msaada wa mablanketi.

Akizungumza kwa niaba ya wanufaika wa msaada wa mablanketi 150, Barakaeli Losaa alisema mara nyingi jamii imekuwa ikiwasahau wazee jambo ambalo limewafanya kuishi maisha magumu.

"Kwa sasa nguvu za kufanya kazi zimepungua sana na tunahitaji msaada kutoka kwa jamii ili tuendelee na maisha yetu. Hata hivyo, jamii imekuwa ikitusahau jambo ambalo limetufanya tuishi maisha ya taabu. Tunaishukuru SBL kwa kuonyesha mfano kupitia msaada huu," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Rais wa Rotary Club ya Mwika, Ester Towo, alisema msaada huo utawasaidia wazee hao katika msimu huu wa baridi na kuongeza kuwa wengi wa wanufaika wamekuwa wakiishi wenyewe pasipo kuwa na msaada.

"Tuna kila sababu ya kuishukuru sana kampuni ya SBL kwa msaada huu wa mablanketi 150. Msaada huu umekuja kipindi muafaka kutokana na kuwa ni msimu wa baridi kali na utawafanya wazee wetu waweze kujikinga na baridi kali haswa wakati wa usiku," alisema.

Meneja wa kiwanda cha SBL Moshi, Alice Kilembe, ambaye alikabidhi msaada huo kwa niaba ya kampuni, alisema, SBL ilikuwa na furaha kuwasaidia wazee wa Mwika. "Msaada tunaotoa leo ni kuonyesha upendo wetu kwa wazee na pia kuthamini mchango wao katika kulijenga taifa wakati wakiwa na nguvu. Jamii ina wajibu wa kutambua mchango wa kundi hili."

Alisema pamoja na msaada huo kwa wazee wa Mwika, kampuni ya SBL pia imekuwa ikitoa misaada mbalimbali kwa jamii katika sehemu tofauti tofauti hapa nchini.

Alitaja baadhi ya miradi ya kijamii ambayo kampuni hiyo inasaidia kuwa ni programu ya ufadhili wa masomo ya kilimo maarufu kama kilimo viwanda ambayo tangu ianze tayari imewanufaisha wanafunzi zaidi ya 200 kutoka katika familia duni.

"Pia tumekuwa tukisaidia miradi ya maji na kuanzia mwaka 2010 tumeweza kuchimba visima zaidi ya 22 ambapo vimezesha watu zaidi ya milioni 2 kupata huduma ya majisafi na salama," alifafanua.

## 'Wajasiriamali kuweni na nidhamu matumizi ya fedha mnazozikopa'

**Na Sabato Kasika**

VIKUNDI vinavyojishughulisha na ujasiriamali vimetakiwa kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha za mikopo inayotolewa na halmashauri ili viweze kupiga hatua na kujiletea maendeleo.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam juzi na Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni kinachopamba na ukatili wa kijinsia, Seleman Bishagazi wakati akitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi vya Kata ya Bonyokwa.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na diwani wa kata hiyo, Tumike Jabir, yalihusisha watu 74 wakiwamo viongozi wa dini, serikali za mitaa na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa kata hiyo Regina Ng'ongolo.

Bishagazi alisema, nidhamu katika matumizi ya fedha, uwajibikaji, muundo wa uongozi wa vikundi, kutunza kumbukumbu na namna ya kuibua na kuandaa miradi ya vikundi ni mambo muhimu kwenye ujasiriamali.

"Mzingatie hayo yote, huku mkikumbuka kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha, kwani baadhi ya watu hukopa na kuzielekeza kwenye mambo mengine badala ya yale waliombea," alisema Bishagazi.

Alisema, wanaofanya hivyo, mwishowe hushindwa kurejesha mikopo na kukwamisha wengine kukopeshwa, kwa kuwa fedha huwa bado ziko mikononi mwao na kuleta msuguano katika vikundi na hata halmashauri.

"Pamoja na hayo, kumbukeni kuripoti vitendi vya ukatili ikiwamo rushwa ya ngono ili kusaidia kukomesha vitendo ndani ya jamii ambayo vimekuwa vikiwagusa zaidi wanawake na wasichana," alisema.

Aidha, Bishagazi alisema kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni kiko chini ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ambapo aligusia umuhimu wa kutoa taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia ikiwamo rushwa ya ngono.

Awali akifungua mafunzo hayo, Diwani wa Kata ya Bonyokwa, Tumike Malilo, alisema amefanya hivyo ili vikundi vijue wajibu wake na kujitathmini kwa ajili ya kusonga mbele kimaendeleo.

"Kwa sasa katika vikundi, usishangae kukuta mwenyekiti anafanya kazi za mhasibu, au kukuta vikundi vingine watu wawili wanapitisha maamuzi badala ya mkutano mkuu wa kikundi," alisema Malilo.

"Diwani huyo alifafanua kuwa lengo lake la kuitisha mafunzo hayo, siyo tu kuwa na uelewa wa ujasiriamali bali pia hata masuala ya haki na nidhamu katika matumizi ya fedha," alisema.

Alifafanua kuwa wanawake na vijana wengi wamekuwa wakifanya biashara huku fedha zao zikiishia kusikojulikana, na kwamba kupitia mafunzo hayo anataka kufungua ukarasa mpya wa uelewa kwa vikundi vya ujasiriamali.

Malilo alisema, mafunzo hayo yatakuwa endelevu kwa muda wa miezi mitatu ambapo kila mwezi yatatolewa mara mbili, huku akitamani kuona kikundi bora wilayani Ilala kinatoka kata yake.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa kata hiyo, Regina Ng'ongolo, alisema mafunzo hayo yamekuja kwa wakati mwafaka, kwa madai kwamba Bonyokwa kumekuwapo na vikundi visivyotimiza wajibu.

"Vikundi hivyo vinatupa shida sisi maofisa maendeleo, lakini mafunzo haya yanaweza kuwa mwarobaini. Nitashirikiana na diwani kuhakikisha vikundi vyote vinapigwa msasa ili kata yetu iwe ya mfano," alisema Regina.

ama
ALHAMISI MEI 5, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

Uhalifu wa kung'oa vibao barabarani unavyoletea madereva majanga ajali



Ukurasa 14

Ulivyo mradi wa kudhibiti Ukimwi na UVIKO -19 ndani ya Polisi, Magereza



Ukurasa 13

Kukosekana maji kulivyo wakala wa magonjwa ya milipuko vijijini

AFYA

# Namna upandikizaji figo mpya unavyochukua nafasi nyingine

• Mganga Mkuu aja na ufafanuzi wake kwa undani

**Na Yasmine Protace**

SHIDA ya kiafya kwenye figo, imo katika orodha ya magonjwa makubwa zaidi hata kuwasababishia watu kupoteza maisha.

Na inapozungumziwa watu wanapoteza maisha, inaangukia katika maana kwamba, ni jambo linalotokana na ama kuchelewa au kucheleweshwa kupata huduma kwenye vituo vya afya, kukitafutwa matibabu sahihi.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, anasema kuchelewa huko kufika kwenye vituo kwa ajili ya matibabu, kuna historia ya kusababisha wengi wao kugundulika na ugonjwa, tena ukiwa wameshafikia hatua mbaya, kwa baadhi ya magonjwa.

Anasema, serikali imekuwa ikiwasisitiza watu kuchunguza afya zao na wanapogundulika kuwa wana matatizo, inakuwa rahisi kwao kuanza kupatiwa matibabu na kuyadhibiti magonjwa tajwa.

Kitaifa, anaeleza kwamba jitihada za serikali katika kupambana kuokoa maisha ya Watanzania wanaosumbuliwa na figo, imewawezesha kuweka mashine za kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo, ikiwamo upandikizaji wa figo.

Katika kuhakikisha inawajali watu ikihudumia katika ugonjwa wa figo, serikali imefunga mashine za kusafisha figo katika baadhi ya hospitali, pia upandikizaji figo.

Dk. Sichalwe anasema ukweli uliopo ni kwamba, usafishaji figo una gharama kubwa kwa mtu, lakini serikali imekuwa ikiingia gharama kubwa katika kuwahudumia wagonjwa hao wa figo.



Baadhi ya wataalamu wa masuala ya afya kutoka nchi tisa za Afrika, wakiwa katika kongamano la kisayansi lililofanyika jijini Dar es Salaam, kujadili ugonjwa wa figo. **PICHA: YASMINE PROTACE**

Pia inaelezwa hadi sasa asilimia 10 ya watu duniani hadi sasa wanaishi na magonjwa sugu ya figo, huku nusu ya watu wenye umri zaidi ya miaka 75, wana magonjwa sugu ya figo.

Ni ufafanuzi wake Mganga Mkuu wa Serikali katika ufunguzi wa kongamano la kisayansi la wauguzi wataalamu wa Afrika lililofanyika jijini Dar es Salaam, akiongeza:.

"Dhima ya kongamano hili ni kuleta maendeleo ya huduma ya magonjwa ya figo duniani na jukumu la elimu na ubunifu kwenye nchi za Afrika na dhima hii, imekuja kwa wakati muafaka ambapo Tanzania inaendua kuimarisha na kupanua upatikanaji wa huduma za figo."

Dk. Sichalwe anabainisha kuwa, hadi kufikia Janauri 31, mwaka huu, kuna jumla ya wagonjwa 2,750 nchini wanaopata huduma ya kusafishwa damu na kufika tarehe hiyo, pia wagonjwa 325 walikwishapandikizwa figo.

Kwa mujibu wa Dk. Sichalwe, wagonjwa 93 wamepandikizwa figo nchini, kati yao waliopatiwa huduma hiyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili wako 67 na Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma, jumla yao 26.

Aidha, Dk. Sichalwe anazitaja hospitali zinazotoa huduma ya kusafisha damu nchini, ni Muhimbili pamoja na hospitali zote za Rufani za Kanda ambazo ni Bugando (Mwanza), KCMC (Kilimanjaro), Benjamin Mkapa na Mbeya.

Nyinginezo anazitaja ni hospitali za rufani za mikoa ya Kagera, Mwanza, Musoma, Kigoma, Arusha, Iringa na Mtwara.

"Ni matumaini yangu kuwa kongamano hili litatusaidia kujua hali halisi ya ugonjwa huu, changamoto tunazokutana nazo katika kutoa huduma za afya ya figo na njia za kuweza kukabiliana nayo," alisema.

Dk. Sichalwe anasema uimarishaji huduma za magonjwa ya figo nchini, unaendana na wauguzi lazima kujipanga katika kuweka jitihada za kupambana na ugonjwa huu hatari, wakiimarisha afya za kinga, kwa kuwa ni njia bora kuliko tiba.

Ni kongamano la kitaalamu, lililojumuisha idadi ya nchi tisa za Afrika, ikiwamo Kenya, Uganda, Misri, Rwanda, Sudan Kusini, Burundi, Ghana, Zambia na wenyeji Tanzania.

AFYA

# Uhalifu wa kung'oa vibao barabarani unavyoletea madereva majanga ajali

**aban Njia,** KAHAMA

- Kote walalama; RTO, Tanroads na madereva
- Vyanzo; madereva wa malori ni vinara zaidi




Magari yakiwa safarini eneo la Tinde, Shinyanga. **PICHA: MTANDAO**

AJALI za barabarani zinatajwa kuchangia vifo vingi vya umma, huku Shirika la Afya Duniani (WHO) linafafanua uzembe barabarani na kushindwa kuheshimu alama za barabarani safarini, kuna mchango mkubwa.

Pia, ripoti ya utafiti uliyofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kukabidhiwa hivi karibuni kwa Wizara ya Mambo ya Ndani, inaonyesha asilimia 70 ya ajali inaanzia kwa madereva.

Kimsingi, madereva wanatuhumiwa kuendesha magari kwa kasi, hata wanashindwa kuyamudu. Pia, kuna suala la kutokufuata sheria na alama za barabarani, huku likijitokeza la kuondolewa vibao vya alama za barabara, zama na wafugaji au wauzaji vyuma chakavu.

Kwa mujibu wa ripoti ya Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani, ni miaka mitatu sasa malori ndiyo yanaongoza kupata ajali, ikilinganishwa na magari mengine yanayofanya safari kati ya mkoa mmoja na mwingine, hawafuati sheria na wanaendesha kwa mwendo kasi, kutokufuata sheria, pia hawatii za barabarani.

Ripoti inayoonyesha mikoa inayotajwa kuongoza matukio ya ajali ni Dar es Salaam, Arusha, Pwani na Morogoro.

## MADEREVA WANAONENA

Raphael Mazigwa, ni dereva wa malori anayefanya safari kati ya Dar es Salaam na nchini Rwanda, anafafanua ukosefu wa vibao vya alama barabarani kwa baadhi ya barabara, zinawasababisha kuvunja sheria za barabara pasipo kufahamu, hata kuma wakati inaishia kuwapo ajali kila mara.

Mazigwa anafafanua kwa kutumia mfano, kila anaposafiri kutoka mkoani Morogoro kwenda jijini Dodoma, kuna baadhi ya maeneo kulikuwapo vibao vya alama vya barabarani, lakini kwa sasa havipatikani, hivyo kwa dereva asiyejua hiyo barabara, inamlazimu kupita kwa kasi na kuna wakati anaweza kuwagonga wanyama.

Pia dereva wa mabasi yaendayo mikoani, Samweli Joramu, anasema barabara za vumbi huwa zinawekwa vibao vya alama za barabarani, tofauti na zenye kiwango cha lami alama ambazo zimechorwa chini, sasa vinapoondolewa inawafanya kukimbia kwa kasi pasipo kuchukua tahadhari.

Dereva Joramu anafafanua, baadhi ya alama za barabarani ni za amri na nyingine ni mahsusi kuonya, sasa wanapozikosa wanalazimika kukimbia kwa kasi bila ya kutambua inapotokea mnyama au mtu anapita, ni mazingira yao kupata ajali.

Katika hilo, anaiomba serikali ijenge desturi ya kuzikagua alama hizo, hata wakazidhibiti ajali. Anaendelea: "Ajali nyingi zinatokea maeneo mbalimbali na lawama tunapewa siye madereva, bila kufahamu chanzo chake ni nini?"

"Tunaendesha vyombo vya moto kwa kufuauta alama za usalama barabarani zinapokosekana tu, tunaendesha kwa tahadhari kubwa sana," anaeleza Joramu.

> **Katika kuondoa ajali za kila mara, wamekuwa wakifanya ukaguzi wa vyombo vya moto kwa namna ya kushitukiza na vile vinavyobainika kuwa na tatizo wanavizuia kusafiri au kuingia barabarani.**



Barabara za Shinyanga na alama zake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

## WATUMIAJI WAONGEA

Michael Bundala, ni mkazi wa Kata ya Nyahanga katika Halmashauri ya Manispaa Kahama, anasema vyuma vinavyobeba alama za usalama barabarani katika maeneo mengi, vimekatwa na wanaokota na kuuza chuma chakavu na wafugaji wa punda, kwa ajili ya kutengenezea mikokoteni inayotumika kusafirishia mazao na pumba.

Anasema, barabara nyingi hazina vyuma vilivyokuwa vimebeba alama za barabara na hiyo imekuwa ikiwasababisha waendeshaji wa vyombo vya moto, wanashindwa kutambua sehemu wanazopaswa kupunguza mwendo kasi, hali inayochangia kuwepo ajali za kila wakati na hasa watoto wadogo.

Mkazi mwingine, Mwasiti Hamisi, anatoa mfano wa barabara inayopitia eneo la Nyahanga inayokatiza aliko Mkuu wa Wilaya ya Kahama na Hospitali ya Manispaa, kulikuwapo vibao kuonyesha alama za barabara, lakini kwa sasa vimeondolewa na magari yamekuwa yakipita kasi, bila kujali wingi wa watu katika eneo hilo.

"Kwa sasa alama za usalama barabarani, zimechorwa tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Hii imewasaidia waendesha vyombo vya moto kupunguza kasi wawapo barabarani kwa kutambua wanahitaji kuchukua tahadhari wawapo safarini," anasema Hamisi.

## TANROADS & RTO

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Mibala Ndilimbi, anasema wamekuwa wakiendelea kuzisimamia barabara zote zilizoko chini yao, kuhakikisha haziharibiwi na watumiaji na kwa anayebainisha kuharibu miundombinu hiyo anawajibishwa kisheria.

Anasema, kuwapo vibao vya alama barabarani vinasaidia kuwaongoza watumiaji wa barabara, wanakotakiwa kuongeza mwendo na kupunguza, ili kuondoa ajali zisizo na ulazima na vinapoondolewa na watu wasiokuwa waadilifu, ndipo zinapotokea ajali za kila mara.

"Vibao vya alama barabarani vinakatwa sana na sijui wanaofanya haya wanakuwa hawatambui umuhimu wa alama hizo?" Analalamika na kukaripia: "Atakayebainika kuhusika na ukataji wa vibao hivyo atakuwa mfano kwa wengine wenye tabia za kukata alama hizo."

Mhandisi Ndilimbi anasema, waondoaji vibao hivyo wamekuwa wakishababishia serikali hasara kubwa, kwa sababu vinapoondolewa, wakati wa virejesha upya ni gharama kubwa, ikilinganisha na namna ya kuvisimika.

Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Shinyanga Mrakibu (SP) Malege Kilakala, anasema katika kuondoa ajali za kila mara, wamekuwa wakifanya ukaguzi wa vyombo vya moto kwa namna ya kushitukiza na vile vinavyobainika kuwa na tatizo wanavizuia kusafiri au kuingia barabarani.

Anasema wamekuwa wakiwachukulia hatua za kisheria madereva wazembe barabarani, kwa kuwatoza faini na wengine wanafikishwa mahakamani.

Pia, anawataka madereva kwenda kusoma na kuzijua sheria zote za usalama barabara, kabla ya kuanza kuendesha vyombo vya moto.

Kamanda Kilakala hata hivyo, anakiri suala la kuondolewa vibao vya alama barabarani, imekuwa kikwazo katika utendaji kazi wa askari wake na kuna yameibuka kwa malumbano baina ya polisi na madereva wakati wa utoaji wa faini, kwa kutokuonekana kwa vibao hivyo ambavyo vinaondolewa na watu wasiokuwa waadilifu.

AFYA

# Kukosekana maji kulivyo wakala wa magonjwa ya milipuko vijijini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

## • Kinamama wanaoyafuata kilomita 15 wasimulia yao



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, akifyatua tofali kwa ajili ya ujenzi wa tangi la maji lita 1,000 linalojengwa katika Kijiji cha Itumbili, Kata ya Chambo. **PICHA: SHABAN NJIA**

SIKU zote inatajwa 'Maji ni Uhai.' Binadamu, mimea na wanyama wanahitaji majisafi na ili kuwa na afya nzuri, kunahitajika majisafi ya kunywa, kupika, pia kwa wanyama na mazao.

Katika hali yake ya asili, maji ni sehemu ya mazingira ambayo wingi na ubora wake, ndio unaosaidia kuamua jinsi maji yatakavyotumika. Upatikanaji majisafi na salama kwa matumizi ya nyumbani na usafi wa mazingira, ni muhimu katika kulinda afya za umma.

Utumiaji maji usio salama, pia uhaba wake unatajwa kuchangia uwapo magonjwa ya milipuko kama vile kuhara na kipindupindu, hususani kwa wanaotumia maji katika mazingira hatarishi.

Kiafya, inaelezwa mtu mwenye afya ya kawaida anaweza kuishi hadi wiki tatu pasipo chakula, lakini kwa maji ni wastani wa siku tatu hadi nne pekee.

Uhalisia wa mwili wa binadamu, ni kwamba hauna uwezo wa kuhifadhi maji muda mrefu na unaendelea kupoteza maji kupitia mmeng'enyo wa chakula, kupumua na kutokwa jasho kadri muda unavyosonga. Hivyo, ni muhimu kurudisha maji mwilini kwa kunywa yaliyo safi.

Imekuwa kawaida watu wanapotembea wanakuwa na chupa za maji ya kunywa, hasa panapokuwapo mazingira ya joto zaidi. Kiafya, maji yanatajwa kuchangia kati ya asilimia 50 hadi 75 ya uzito wa mwili wake na muhimu, kwa sababu imeitwa chanzo cha uhai.

### WANANCHI VIJIJINI

Maisha Raphael, mkazi wa kata ya Mwanase katika Halmashauri ya Msalala, anafafanua kwamba wanalazimika kutumia maji ya visima walivyochimba wao, kwa kuchangia na mifugo yao wanaoyafuga, baada ya ukosefu wa huduma ya majisafi na salama.

Raphael anafafanua, wanaendelea kupata magonjwa ya mlipuko kila wanapotumia maji hayo, hususani kwa watoto wengi ambao ni wanafunzi, hivyo anaiomba serikali ihimize makandarasi kukamilisha kwa wakati miradi ya maji inayojengwa katika maeneo yao.

Anasimulia kuna wakati wamekuwa wakiamka alfajiri na kufunga safari hadi kata za jirani kwenda kuteka maji na kasha wanarejea majumbani saa tatu asubuhi, wakiwa wanakutana na vikwazo vikubwa vikiwamo vya kunusurika kushambuliwa na wanyama kama fisi.

Mariam Simon, naye anasema wao wanalazimika kutembea umbali wa kilomita 15 kwenda na kurudi kutoka kata za Mwanase na Kashishi kuchota maji visimani na kwa wasio na uwezo wa kufika huko, wanalazimika kununua maji ndoo lita 20 kwa bei Sh.1,000.

"Kwa sasa kila ugonjwa unaotokea kwenye maeneo yetu tunajua ni magonjwa yatokayo na kutumia maji machafu. Licha ya kuyatumia hivyo hivyo, tunajitahidi kuyachemsha kabla ya kuyatumia, ili tuendelee kuwanusuru watoto wetu na magonjwa hayo hatari," anasema Simon.

### WAHUSIKA RUWASA

Wakala wa Usambazaji wa Maji Vijijini (RUWASA), katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, asasi

imejenga na kukamilisha jumla ya miradi 652 ikiwa na vituo vya kuchota maji 11,457 inayohudumia vijiji 1052 na kunufaisha wananchi wapatao 3,824,914.

Aidha, wananchi wanaoishi pembezoni mwa miji wanatajwa kuendelea kupata magonjwa ya mlipuko, hususani kipindupindu, baada ya kutumia maji yasiyo safi na salama kiafya. Hiyo ni baada ya kutumia maji ya kwenye madimbwi na visima walivyochimbwa jirani na makazi yao.

Paschal Mnyeti, ni Kaimu Meneja wa RUWASA Kahama, anayetaja jitihada za namna ya kukabili hali hiyo, hadi sasa serikali imendelea kutenga fedha na kutekeleza miradi ya maji katika maeneo mengi hapa nchini.

Anafafanua, katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama kuna miradi ya maji inayoendelea kutekelezwa yenye thamani shilingi bilioni nne, lengo ni kuwasogezea huduma ya majisafi wananchi ambao wameanza kutumia maji ya Ziwa Victoria.

Vilevile, anasema kuna wananchi 12,488 kutoka kata nne za Halmashauri ya Msalala, wanatarajia kunufaika na mradi wa maji kutokaa Ziwa Victoria unaotekelezwa RUWASA kwa shilingi bilioni 2.035 ili kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

Anawataja wananchi hao ni kutoka katika vijiji na kata zake katika mabano; Mwakuzuka (Mwanase), Kabondo (Kashishi), Izuga (Jana) na Mwashigina (Mwakata), mpango uliopo kila kijiji kitajengewa gati la maji lenye ujazo wa lita 90,000 na umma kuuziwa maji kwa bei nafuu wanayomudu.

Mnyeti anasema tayari kunavijiji viwili vinaendelea kunufaika na majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria kwa kujengewa magati mawili ya shilingi milioni 821 na wananunua maji kwa bei ndoo ya lita 20 kwa shilingi 50.

> **Tayari kunavijiji viwili vinaendelea kunufaika na majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria kwa kujengewa magati mawili ya shilingi milioni 821 na wananunua maji kwa bei ndoo ya lita 20 kwa shilingi 50.**

Mhandisi Mnyeti anasema, ugumu wanaoupata kutoka kwa makandarasi ni wanaposhindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati, sababu kuu ni kucheleweshwa malipo yao kwa wakati, kabla ya kuendelea na awamu nyingine iliyopangwa.

### DC & MAKANDARASI

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, anatahadharisha wanaoshindwa kufanikisha miradi kwa wakati, watanyimwa kandarasi.

Anatoa mfano, kuna baadhi ya miradi ya maji katika Halmashauri za Msalala na Ushetu, ilianza ujenzi wake tangu mwaka 2018 nayo haikukamilika kwa wakati katika mazingira kama hayo.

Mkuu wa Wilaya anafafanua tahadhari yake kwamba, hatosita kuwachukulia hatua za kisheria makandarasi wanaotekeleza miradi yao kwa kutozingatia muda, wakazi wakiendelea kuteseka na hali ngumu.

"Nahitaji miradi yote ya maji inayoendelea kujengwa wilayani kwangu ikamilike... nje ya hapo nitawajibisha makandarasi kwa kuwanyang'anya tenda na kuwapiga marufuku kupata tenda nyingine, labda mpaka nitakapoondoka wilaya hii," anasema Kiswaga.

Katika hilo, mwakilishi wa makandarasi wanaotekeleza miradi ya maji Ushetu, Mhandisi John Panga, anasema maagizo ya Mkuu wa Wilaya wameyapokea na watahakikisha kwa muda uliotolewa miradi yote ya maji, itakuwa imeekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

AFYA

# Ulivyo mradi wa kudhibiti Ukimwi na UVIKO -19 ndani ya Polisi, Magereza

## • Vituo afya kitaifa vyaongezewa uwezo

Na Maulid Mmbaga

JESHI la Polisi nchini Kitengo cha Afya, kwa kushirikiana na Taasisi ya Tanzania Health Promotion Support (THPS), sasa wanaendeleza jitihada kudhibiti Virusi vya Ukimwi na janga la UVIKO-19 kwa polisi na jamii zao, kwa ujumla nchini.

Zaidi ya wiki mbili zilizopita, taasisi hiyo na polisi walizindua kampeni katika Hospitali ya Polisi, iliyoko Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.

Ukiwa chini ya ufadhili wa Shirika la Misaada ya Kimataifa la Marekani (USAID), mradi huo ni wa Polisi na Magereza, unalenga kuongeza kasi ya upatikanaji chanjo za UVIKO-19. Mkakati unawalenga askari polisi, familia zao na jamii inayohudumiwa katika vituo vya afya 28 vya jeshi hilo, pia vitano vya mafunzo yao kitaifa.

### MSIMAMIZI MRADI

Mkurugenzi Mtendaji wa (THPS) Dk. Redemta Mbatia, anaiambia Nipashe, kampeni inatazamia kusaidia mpango wa kitaifa wa kuongeza kasi ya utoaji chanjo ya UVIKO-19, kwa kuongeza idadi ya wateja wa chanjo hiyo katika vituo vya afya vya polisi.

Pia, anafafanua mwelekeo wao wataendelea katika vyuo vitano vya Polisi vilivyoko Dar es Salaam, Kidatu, Mwanza, Moshi na Zanzibar. Kwa sasa, huduma hiyo inatolewa katika vituo vyote 28.

Dk. Redemta anaeleza dhima ya kampeni hiyo, ni kusaidia kuunda mahitaji ya nyenzo za elimu, ili kuuongeza ufahamu wa jamii, umuhimu wa chanjo na kutoa mafunzo kwa wahudumu afya, kuhusu uhamasishaji unaosaidia uanzishaji chanjo.

Pia, mengine yanagusa kusaidia timu za usimamizi wa afya na jamii katika kufuatilia utoaji huduma za chanjo katika maeneo yao, wakisimamia na kushauri ujumuishaji wa utoaji huduma ya chanjo ya UVIKO-19 katika huduma ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na kifua kikuu kwenye vituo na uhamasishaji wa jamii.

"Malengo ya mradi ni kuhakikisha afya za Watanzania hususani askari na familia zao, wafungwa na jamii inayowazunguka zinaimarika kupitia uimarishaji na upatikanaji wa huduma zenye ubora katika afua za kuhudumia, kudhibiti na kutibu magonjwa yatokanayo na Ukimwi na kifua kikuu," anafafanua.

### UDHIBITI ULIVYO

Anasema, mradi huo wa Polisi na Magereza umo katika yanayotekelezwa na THPS, ikishirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Wizara ya Afya.

Dk. Redemta anaeleza mradi mwingine ni wa kupambana na Ukimwi na uko katika mikoa ya Pwani, Kigoma na Shinyanga, walioingia mkataba naWizara ya Mambo ya Ndani, pia USAID.



Sehemu ya mandhari ya Hospitali ya Polisi, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

> **Tumekuwa tukienda na kuangalia mapungufu yaliyoko ili kuhakikisha kwamba tunapowajengea uwezo uwe unatatua changamoto iliyopo.**




Ni mkakati unaolenga vituo 64 vilivyoko katika halmashauri 35 za Tanzania Bara na Zanzibar; vituo 28 vya polisi na 36 vya Magereza, wakishirikiana na Kikosi cha Afya Kuu na Afya na Lishe cha Magereza.

### HATUA ZA MAFANIKIO

Dk. Redemta anasema, ni mradi unaoajiri watumishi na kufungua ofisi nne za kanda zilizoko Dodoma, Dar es Salaam, Kilimanjaro na Mwanza, wakiwa na angalizo la hitaji muhimu la nguvukazi, kuhakikisha huduma bora zinapatikana.

Hapo Dk. Redemta anafafanua, wana nafasi ya kuajiri watumishi zaidi ya 40 kati mgawanyiko; wauguzi 17, madaktari sita na maofisa takwimu 17, walioko vituo kusaidia utoaji huduma.

Dk. Redemta anaeleza, pia kuna waelimisha rika 103 wa kujitolea waliopewa mafunzo na sasa wanahudumia, kuhakikisha wateja wapya wenye kifua kikuu na Ukimwi wanaibuliwa na wanatibiwa.

Anasema, hilo linaendana na kuhakikisha wanadumu katika tiba kwa kuwafuatilia watoro majumbani, ili watumie dawa kwa usahihi.

"Tumekuwa tukienda na kuangalia mapungufu yaliyoko ili kuhakikisha kwamba tunapowajengea uwezo uwe unatatua changamoto iliyopo," anaeleza Dk. Redemta.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, mradi pia unafuatilia kila mwezi, huku wasimamizi maalum, sambamba na Kikosi cha Afya cha Polisi na Kitengo cha Afya Lishe, wakitathmini mwenendo husika, kulingana na malengo ya mradi ya mwaka.

Pia mradi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya unaendelea kuwezesha na kuendesha mafunzo ya afya 14 za Ukimwi na kifua kikuu, kwa watumishi wa vituo husika.

Kuhusu Uviko 19, anasema mradi unafanya kazi na serikali kudhibiti maambukizi kwa watumishi 102 na waelimisha rika 103 kuwawezesha katika uelewa jinsi ya kujikinga na kusaidia upatikanaji barakoa, vitakasa mikoni, ndoo za kunawa mikono na sabuni.

Dk. Redemta, anabainisha wamenunua vifaa tofauti vya kuboresha huduma katika vituo 64, kusaidia mafunzo ya masafa na mawasiliano, vitakavyosaidia utoaji mafunzo kwa watumishi kwa njia ya mtandao.

"Uimarishaji wa utoaji wa huduma kwa mwezi Julai 2021 hadi Machi 2022 wateja wapya 2164 wamegundulika kuwa na maambukizi ya VVU na kuunganishwa katika huduma ya tiba na matunzo ya dawa kwa mwezi na wateja 1286 walioripotiwa kupotea wamerudishwa," anasema Dk. Redemta.

Anasema kwamba, kuna uhaba wa watoa huduma wa afya waliopata mafunzo sahihi kuhusu maradi kama Ukimwi na kifua kikuu. Pia, anataja kasoro katika hali ya miundombinu, akidai kuwa nafasi katika vituo vyao vya afya bado ni finyu na iliyopo, iko katika hali chakavu inayohitaji kukarabatiwa.

### WITO KWA POLISI

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Jumanne Muliro, anawaahidi THPS watashirikiana nao kuhakikisha wanalinda afya ya polisi na familia zao, pia jamii.

Anaseme wanatambua kuwa suala la chanjo ni la hiyari lakini kwa sababu bado wanawahitaji polisi watamshangaa sana askari ambaye hajachanja na bado anaingia katika makundi ya kujadiliana ambayo hayana mwelekeo mzuri wa kisayansi.

"Hakuna serikali inayoweza kumtanguliza askari kwamba tunataka tumuue, sasa akifa askari ulinzi utakuwa wa nani? Mimi nasisitiza kama kuna askari yoyote hajachanja kwa sababu za uzembe au kutojali kama binadamu kusema kweli simwelewi.

"Tuchanje wale ambao hatujachanja kwa afya zetu. Huwa tuna misemo sisi katika jeshi kuwa mtu hawezi kufa mara mbili ukifa unakufa mara moja, kwahiyo chanjo ni umuhimu sana. Haiwezekani serikali ikasisitiza masuala ya chanjo, halafu wewe ukawa bado unasita," anasema SACP Muliro.

Mratibu wa VVU na Ukimwi Kitengo cha Afya Polisi, Thomas Kawala, anaeleza katika upanuzi wa utoaji huduma hiyo, wataendelea kuwaomba askari wajitokeze na familia zao, kutathminiwa na afya zao na kutibiwa, ana fafanua kuwa wanaweza kutengeneza miradi ya pamoja inayohusu afya, wakiwalenga askari na familia zao.





## Kongamano kupokea maoni mitaala elimu, Sera ya Elimu 2014

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepanga kufanya kongamano kubwa la elimu nchini mwishoni mwa mwezi huu litakalokwenda sambamba na kupokea maoni zaidi kwa ajili ya kuboresha mitaala ya elimu na Sera ya Elimu ya mwaka 2014.

Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda, alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mageuzi makubwa ya sekta ya elimu nchini.

Alisema pia wizara itaendesha kongamano hilo ambalo litafanyika kwa siku tatu kwa ajili ya kupata maoni zaidi sekta hiyo.

"Kongamano hilo litafuatiliwa na kongamano la kimataifa la Afrika Mashariki na mkutano wa kimataifa wa mageuzi ya elimu utakaofanyika New York nchini Marekani," alisema.

Hata hivyo, alisema wizara imepanga kukutana na wabunge Mei 7, mwaka huu ili kuwapa fursa ya kutoa maoni yao kwa ajili ya maboresho hayo.

"Mkakati wa serikali ni kufanya maboresho makubwa ya sera na mitaa ya elimu ambayo yatajikuta katika elimu ujuzi, Mei 7 mwaka huu tutakutana na wabunge ikiwa ni mwendelezo wa kupokea maoni ya kuboresha mitaala na sera ya elimu," alisema.

Waziri Mkenda alisema chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan yatafanyika mageuzi makubwa ya elimu ambayo hayajawahi kutokea tangu Tanzania ipate uhuru ambapo rasimu ya mitaala mipya itatoka Mwezi Desemba mwaka huu.

"Kazi kubwa ya mitaala imefanyika na tumekusanya maoni zaidi ya 100,000, lakini ukikutana na mtu anakuuliza mnafanya nini kwenye elimu, sasa kutakuwa na makala kwenye televisheni,"alisema.

Alisema rasimu hiyo itapelekwa kwenye maamuzi serikalini na awali ilipangwa kuanza kutumia mitaala iliyoboresha Mwaka 2026 lakini kwa kasi waliyonayo utekelezaji wake utaanza Mwaka 2024 kwa awamu.

# Bajeti masuala ya ubunifu yaongezwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imepanua wigo wa bajeti ya masuala ya ubunifu nchini kutoka Sh. bilioni moja kwa mwaka 2021/22 hadi kufikia Sh. bilioni 5.5 kwa mwaka ujao wa fedha 2022/23.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Eliamani Sedoyeka, aliyasema hayo jana kwenye ufunguzi wa mafunzo kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Dodoma kuhusu Wiki ya Ubunifu Tanzania 2022 iliyoandaliwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kupitia mradi wake wa FUNGUO.

Alisema katika bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambao unaishia Juni 30, mwaka huu, kiasi cha Sh. bilioni moja kilitengwa kwa ajili ya kuendeleza wabunifu.

"Fedha hizi zipo COSTECH (Tume ya Taifa Sayansi na Teknolojia) na tayari wapo wabunifu ambao wamepokea na wanaokwenda kupokea," alisema.

Alieleza kuwa kwa mwaka ujao (2022/23), serikali imepanga kutenga Sh. bilioni 5.5 kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi ya kubuni na kuendeleza bunifu, kujengea uwezo taasisi na mbunifu mmoja mmoja.

"Mtu akifanya bunifu tunamshauri sana kwenda serikalini kulingana na ubunifu wake, lakini Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kushauri viwango vinavyotakiwa kulingana na ubunifu uliobuniwa, pia bunifu zifanywe kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi," alisema.

Hata hivyo, alisema hadi sasa wabunifu ambao wametambuliwa, kuziangalia teknolojia na kuziingiza kwenye vituo atamizi kwa matumizi ya nchi ni takribani 200 na Sh. bilioni 2.3 zimetumika kuendeleza gunduzi zao.

"Kati ya bunifu ambazo zimefanya vizuri sana ni Magila Tech alianzia akiwa mwanafunzi IFM na kwenda COSTECH pale akapewa support na serikali sasa hivi yeye ni kati ya wabobezi duniani katika usalama wa mitandao, na juzi amefungua ofisi Dubai ikiwa ni ofisi yenye vijana wa kitanzania saba, NIT pia wameshatengeneza gari, nimeona Kipanya ametengeneza gari, ukienda Arusha Tech imetengeneza gari ndogo kwa ajili ya wenye changamoto za kutembea kwa miguu, ambayo inatumia umeme jua,"alisema.

Aidha, alisema sayansi na teknolojia ni muhimu duniani kote katika kuchochea kasi ya kimaendeleo, kiuchumi na kijamii.

Alisema kwa kuweka mfumo wa elimu vizuri unawezesha kutengeneza wanasayansi mbalimbali ambao kwa kutumia ubunifu wanaweza kutengeneza teknolojia ambazo zitatumika katika kupiga hatua za kimaendeleo.

Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara hiyo, Prof. Maulilio Kipanyula, alisema kwa mwaka huu wanafunzi 50 wa shule za msingi wameomba kushiriki Wiki ya Ubunifu mwaka huu.

"Tumepanua wigo wa wa kuwatambua kupitia maofisa maendeleo ya jamii, na tumeshawafundisha wawe ni kiungo kule chini ili wakiibuliwa wabunifu watambuliwe kuanzia ngazi ya chini," alisema.

Kadhalika, alisema Wiki ya Ubunifu na Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) itaanza Mei 15 hadi 20, mwaka huu jijini Dodoma ambapo imedhamiria kuhamasisha ubinufu, sayansi na teknolojia.

"Tumehamasisha Wiki ya Ubunifu kwa ngazi mbalimbali ambapo kwa mwaka huu tumehamasisha mikoa 16, ambapo kutakuwa na shughuli mbalimbali zinazolenga kuadhimisha wiki ya ubunifu mwaka huu, mikoa hiyo ni Dar es salaam, Dodoma, Mbeya, Arusha, Iringa, Mwanza, Zanzibar, Tanga, Kilimanjaro, Njombe, Kagera, Mtwara, Mara na Ruvuma, lengo ni kuhamasisha ubunifu,"alisema.

Alisema kwenye wiki hiyo kutakuwa na majukwaa ya majadiliano kuhusu maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu nchini, kuwapo kwa mafunzo ya elimu ya ujasiriamali kwa wabunifu ili kuwa fursa ya kiuchumi na kutengeneza ajira.

Meneja Mradi wa FUNGUO Innovation kutoka UNDP, Joseph Manirakiza, alisema mradi huo umejipanga kuendeleza masuala ya ubunifu kwa kuwasaidia wabunifu ambao bunifu zao zinataka kuingia sokoni lakini wana tatizo la kifedha.



Mkurugenzi Mtendaji na Mratibu Mkuu wa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (MKURABITA), Dk. Seraphia Mgembe, akizungumza na wakazi wa kijiji cha Msisi wilayani Bahi mkoani Dodoma mapema wiki hii, kuhusu umuhimu wa kuwa na hati ya mashamba. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Bahi washauriwa kutambua umuhimu hati za mashamba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKAZI wa Wilaya ya Bahi, wameshauriwa kutambua umuhimu wa hati za mashamba kama ufunguo wa kuondokana na umaskini.

Mkurugenzi Mtendaji na Mratibu Mkuu wa Mpango wa Kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA), Dk. Seraphia Mgembe, ndiye aliyetoa ushauri huo juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa Vijiji vya Msisi na Makanda vya wilaya hiyo kuhusu umuhimu wa elimu wa kuwa na hati za miliki za mashamba ili kujiepusha migogoro ya ardhi.

"Naomba msibaki nyuma kutumia fursa ya urasimishwaji wa mashamba unaofanywa na serikali, changamkieni fursa ya kupata hati za mashamba mliokuwa nayo ili kuondokana na bugudha ya hapa na pale," alisema.

Alisema kukabidhiwa kwa hati wameshajikwamua kimaendeleo hivyo wasikubali kubaki nyuma na badala

wahimize na wengine ambao hawana uelewa juu ya kuwa na hati ili wajitokeze kuchangamkia fursa hiyo.

"Tunaamini elimu tuliyotoa italeta matokeo chanya, kwa sababu tumewajengea uwezo halmashauri ili zoezi la urasimishaji liwe endelevu katika maeneo ambayo yamebakia,"alisema.

Diwani wa Kata ya Msisi, Mathayo Malilo aliishukuru serikali kwa kuwapatia hati za mashamba wanakijiji wa eneo hilo na kuomba kuwapa elimu wananchi ili kutumia hati hizo kukopa mikopo ya kuendeleza kilimo.

Alisema wananchi wengi wanauelewa mdogo hivyo wakipewa elimu ya mikopo na umuhimu wa kuwa na hati itawasaidia kwa kiasi kikubwa kuhakikisha wanainuka kiuchumi wao na familia zao.

Mbunge wa Bahi, Kenneth Nollo, alisema serikali kutokana na kuwajali wananchi wa eneo hilo anaomba kuendelea kurasimisha mashamba ya wanakijiji katika maeneo ambayo bado.

Alisema wanakila sababu ya kufurahi kupata hati kutokana na kwamba itasaidia kupunguza migogoro ya ardhi pamoja na kuwapa fursa wakazi wa maeneo hayo kupiga hatua kimaendeleo.





Baadhi ya madereva bajaji jijini Mbeya, wakiwashusha abiria jana, katika kuendeleza mgomo wa kushinikiza kupandishwa kwa nauli kutoka 500/- hadi 1,000/- baada ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji nchini (EWURA) kutangaza bei mpya za mafuta. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Uhasama madereva wa bajaji, daladala wazikwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UHASAMA baina ya madereva wa bajaji na daladala zinazotoa huduma katikati ya Jiji la Mbeya umezikwa rasmi kutokana na ongezeko la bei za mafuta.

Madereva hao kwa muda mrefu walikuwa na uhasama wakigombea njia za kutoa huduma, hali iliyokuwa ikisababisha kuibuka kwa migomo ya mara kwa mara kwa vyombo hivyo vya usafiri.

Katika kuonyesha kuwa uhasama umezikwa, jana madereva wa bajaji waliandamana kushinikiza madereva wa daladala kupandisha bei za huduma zao kutoka Sh. 400 wanazowatoza abiria wao kutoka kituo kimoja hadi kingine na kuwa Sh. 1,000 ili ifanane na ambayo inakusudiwa kutozwa na madereva wa bajaji.

"Tunaomba wenzetu wa daladala tuwe kitu kimoja bei za mafuta zimepanda hivyo nasi tupandishe nauli kutoka Sh. 400,500 hadi 1,000, ili kufidia gharama za mafuta ambazo kwa sasa hazikamatiki," alisema mmoja wa waendesha bajaji.

Akizungumza na Nipashe, Chuma Saanane, alisema madereva wa vyombo hivyo wanapaswa kuwa kitu kimoja ili kukabiliana na mfumuko wa bei za mafuta ambazo zimechangia kupanda kwa gharama za maisha.

Alisema hata kama madereva daladala wakigoma kupandisha nauli wao wataendelea na msimamo wao kutumia nauli ya Sh. 1,000 hadi mamlaka zitakapotangaza kushuka kwa bei za mafuta nchini.

"Abiria wanakataa kulipa nauli ya Sh. 1,000 kwa madai kuwa gharama imekuwa kubwa mno na hali ya maisha imekuwa ngumu hivyo kulipa kiasi hicho ni ngumu, wakati huku bei ya mafuta imepaa pia tunapitia wakati mgumu sana," alisema Saanane.

Mwenyekiti wa Umoja wa madereva bajaji na wamiliki Jiji la Mbeya, Festo Mwasimba, aliwaomba madereva kusitisha maandamano hayo wakati wakisubiri serikali kutoa utaratibu mwingine ili kupunguza makali ya kupanda kwa bei za mafuta.

Alisema mgomo na maandamano kushinikiza kupandisha nauli hakutasaidia badala yake serikali na madereva wakae pamoja kuangalia namna kumaliza suala hilo kwa manufaa ya pande zote.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi, Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Nishati na Maji nchini (EWURA) kwa Mkoa wa Mbeya, bei ya mafuta ya petroli imepanda kutoka Sh. 2,969 hadi 3,271 kwa maeneo ya Wilaya ya Kyela na Chunya.

Bei ya dizeli kwa sasa ni Sh. 3,381 kwa Wilaya za Kyela na Chunya huku Mbarali ikiwa Sh. 3,239 wakati huo huo mafuta ya taa ikifika hadi Sh. 3,235 katika baadhi ya maeneo.

# Walioshindwa kurudisha mkopo kusakwa nyumba kwa nyumba

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, imetangaza msako wa nyumba kwa nyumba, kuvisaka vikundi vyote vilivyokopa na kushindwa kurejesha mikopo yao iliyofikia Sh. bilioni 1.5.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Twalibu Lubandamo, alitoa kauli hiyo juzi, kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichokuwa na lengo la kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo.

Lubandamo alisema, msako huo unaanza mara moja ili kuwakamata wadaiwa wote waliokopa, kwa kuwa fedha hizo zinatakiwa kurejeshewa ili watu wengine waweze kukopa.

"Kiasi cha bilioni 1.5 ambazo ni fedha za mikopo kilichotolewa na halmashauri ikiwa ni asilimia 10 kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, hadi sasa hakijarudishwa hali inayosababisha vikundi vingine kushindwa kunufaika," alisema Lubandamo.

Kutokana na hali hiyo, alisema watahakikisha vikundi vyote vilivyokopa vinarejesha kwa usimamizi wa Jeshi la Polisi Kata, ambao watazifikia kata zote kuhakiki wadaiwa.

Diwani wa Igurusi, Hawa Kihwele, alisema mikopo hiyo inayokopeshwa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, fedha zinatokana na mapato ya ndani ya halmashauri hiyo.

Kihwele alisema, inasitikisha kuona wakopaji wanaona fedha hizo kama zawadi wakati wanatakiwa kurejesha ili vikundi vingine viweze kukopa.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Missana Kwangura, alisema anabariki maazimio ya baraza la madiwani kuwasaka nyumba kwa nyumba wadaiwa wote ili kusaidia Sh. bilioni 1.5 zilizokopwa na vikundi vyote kurejeshwa.

"Uamuzi huu kamati ya fedha naubariki kwa sababu utaongeza msukumo wa kurejesha fedha zilizokopwa na baadhi ya vikundi, inaumiza kuona fedha hizi ambazo hazina riba zinachezewa na wachache wasiokuwa waungwana naowamba madiwani nguvu yetu ikasaidia kufanikisha jambo hili," alisema Kwangura.

# Mbunge akabidhi mtungi wa kuchakata mawe wa milioni 9.5/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Maji ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, amekabidhi mtungi wa kuchakata mawe ya dhahabu (karasha), wenye thamani ya Sh. milioni 9.5 kwa umoja wa wanawake Chunya ili uwasaidie kujikwamua kiuchumi.

Mhandisi Mahundi alikabidhi karasha hilo juzi na kusema mradi huo ni utekelezaji wa ahadi yake kwa wanawake hao ili kuwasaidia kukuza uchumi wao.

"Nilitoa ahadi kwa wilaya zote za Mkoa wa Mbeya kuzipatia miradi yenye thamani ya Sh. milioni 20 na kwa kuanzia nimeona nianze na Chunya ambao wao walichagua mradi wa karasha wenye thamani ya Sh. milioni 9.5, huu ni mwanzo tu tutafanya mambo mengi kwa pamoja," alisema Mhandisi Mahundi.

Akishukuru kwa niaba ya Umoja wa wanawake wa Chama Cha Mapinduzi CCM, Zaituni Sembo, alisema kuwa Wilaya ya Chunya walichagua mradi wa karasha ambalo litakuwa linasaga mawe walilopatiwa na mbunge.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, aliutaka uongozi wa Umoja wa wanawake wilayani humo kutafuta eneo ambalo halina migogoro litakalowekwa mtungi huo wa kusaga mawe.

"Mradi huu, naomba uwe endelevu, mkishirikiana na kuwa kitu kimoja hakika mtapiga hatua na mtatajirika kwa sababu kumiliki karasha la madini sio jambo dogo, tunamshukuru Naibu Waziri kwa kuwapatia kitu chenye thamani," alisema Mayeka.



# Madaktari wakumbushwa huduma bora

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKE wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Sharifa Omar Khalfan, amewataka madaktari wa Hospitali ya Wilaya ya Kivunge Mkoa wa Kaskazini Unguja kuendelea kutoa huduma bora ili kusaidia kuimarisha afya za wananchi.

Sharifa aliyasema hayo jana baada ya kufanya ziara hospitalini hapo akiwa na viongozi wengine kuwajulia hali wagonjwa na kuwapa zawadi za Eid el Fitri.

Alisema serikali inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi imedhamiria kuboresha huduma za afya ili wananchi wake wapate huduma bora.

Sharifa alitaja lengo la kwenda hospitalini hapo kuwa ni kuwafariji na kuungana na wagonjwa katika sikukuu hiyo ili kuzidisha umoja, mshikamano na mapenzi baina ya Wazanzibar.

“Ninapongeza madaktari wa hospitali hii kwa kujitolea kuwahudumia wagonjwa hatua ambayo inaongeza imani ya serikali kwa watumishi wa kada ya afya,” alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhamed Mahmoud, alisema ziara hiyo ni ya kwanza kufanyika mkoani humo na alimshukuru mke huyo wa Makamu wa Pili wa Rais kwa kuwatembelea wagonjwa.

Kuhusu matatizo ya upatikanaji wa dawa za ganzi kwa wagonjwa wa kisukari alisema atalisimamia ili zipatikane kwa wakati na za kutosha.

Viongozi wengine waliojumuika naye ni pamoja na Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Khadija Shamte ambaye alisema kuwa tume ina mkakati wa kuanzisha Sheria ya Bohari ambayo itasaidia wananchi kupata huduma ya dawa kwa urahisi zaidi.

## Mpango wa serikali wawatia wasiwasi wakulima mwani

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya wakulima wa mwani wameeleza wasiwasi wao kuhusu mpango wa serikali wa kutofautisha maeneo ya wakulima wa zao hilo na ya watalii.

Wakizungumza katika mkutano wa kuwasilisha utafiti wa kuwajenga uvumilivu wakulima hao uliowasilishwa na Meneja Miradi kutoka Milele Zanzibar Foundation, Ali Rashid, walisema kutokana na maumbile ya ulimaji wa zao hilo ni ngumu kutengewa maeneo yao.

“Wakulima wa mwani tuna tabia ya kuhama hama kwa kulingana na hali ya uzalishaji wa zao hili, kwa mfano unapolima kuna muda uzalishaji unapokuwa mzuri tutaendelea nalo na kama siyo mzuri huwa tunaondoka na kwenda eneo lingine,” Mwanaisha Makame kutoka Paje alisema.

Makame alisema iwapo kutakuwa na mgawanyo wa maeneo badala ya kuongeza uzalishaji itasababisha kupunguza zao hilo na uzalishaji wake.

Akitolea ufafanuzi wa suala hilo, Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Sheha Idrissa, alisema wakati wa utekelezaji wake watashirikisha wadau wote.

“Serikali inajali mchango wa wakulima na ndiyo maana wanajitahidi kupanga mipango mbalimbali ya kuhakikisha wanaendeleza ukulima wao bila ya vikwazo,” alisema.

Akiwasilisha utafiti wao, Rashid alisema upandaji wa zao la mwani una kazi kubwa lakini malipo ambayo wanayapata ni madogo ikilinganishwa na kazi wanayoifanya katika ukulima wake.

Pia alisema sekta hiyo ya mwani ina matatizo mengi ambayo kuondoka kwake ni lazima kuandaliwe mijadala mbalimbali itakayoweza kutoa mafanikio yake na kuliletea heshima zao hilo.

Zanzibar ni miongozi mwa nchi nne duniani zinazozalisha mwani nyingi ambapo mpaka sasa inadaiwa kuna maeneo 83 yanayotumika kulima ambayo serikali imekuwa ikipita na kutoa elimu ya ukulima bora.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud (kulia), akisalimiana na Makamu wa Rais mstaafu, Dk. Muhammed Gharib Bilali, baada ya kumalizika kwa sala ya Eid El Fitr katika msikiti wa Zinjibar Mazizini Zanzibar juzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jamii yahimizwa malezi ya yatima

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZAINAB Kombo ambaye ni mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, amesema wanajamii wana jukumu kubwa la kuwalea watoto yatima ili kupata faraja kama wengine.

Kauli hiyo aliitoa juzi katika hafla ya chakula cha mchana kilichoandaliwa na Zanzibar Noor Foundation kwa ajili ya watoto yatima.

Alisema kila mwananchi kwenye jamii yake ambaye anaishi na watoto yatima atambue kuwa ana jukumu la malezi yao.

Zainab alisema vyema watoto hao waonyeshwe mapenzi na furaha kama wengine kwa sababu hatakiwi kujiona wanyonge wala wenye kukosa furaha.

“Hawa watoto kwetu ni mtihani wa Mwenyezi Mungu anatupima hivyo tusifeli katika mtihani huu, tuwaangalie kama anavyotuwezesha katika kuwatunza na kuwalea kama watoto wengine,” alisisitiza.

Zainab ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo alisema imekuwa ni kawaida kwao kukaa pamoja na watoto hao kufurahi nao baada ya waislamu kumaliza mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma aliipongeza jumuiya hiyo kwa kitendo hicho walichokifanya cha kukaa na watoto hao ili nao wafurahie siku hiyo muhimu.

Alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuwalea watoto hao kama dini inavyoelekeza na ikibidi kulelewa katika familia badala ya vituoni.

“Kukosa ubinadamu kunatufanya baadhi ya watu kutowajali watoto hawa jambo ambalo siyo zuri,” alisema.

Aliwaomba wazee wenye watoto hao wasikae kwa unyonge kwa sababu serikali yao inawasimamia pamoja na jumuiya mbalimbali katika kuwajali watoto hao. Ukhty Amina Salum ambaye ni mwanaharakati katika masuala ya wanawake na watoto alisema watoto hao ni muhimu kukaa nao pamoja na kuwasimamia ili kuona wanakuwa na furaha wakati wote.

Aliwaasa wananchi kuacha kula mali ya yatima na kuogopa katika jambo hilo ambalo lina dhima kubwa kwa Mungu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

EQUITY FOR TANZANIA LTD wanatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye namba za usajili T 572 DFH, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa ARU/ARU/RB/162679/2022

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA BUKOBA MJINI MKOA WA KAGERA.**
**Shauri la Mirathi Na. 15/ 2019**
**Msimamizi 1. HASHIMU ABDALLAH**
**Msimamizi 2. MUNIRA ABDALLAH**

**KUITWA SHAURINI MSIMAMIZI WA MIRATHI KWA HASHIMU ABDALLAH MSIMAMIZI WA MIRATHI**
Kwa kuwa MUNIRA ABDALLAH ameleta madai yake kwamba HASHIMU ABDALLAH hatoi ushirikiano kuhusu kugawa mirathi na anafaidika peke yake na mirathi hiyo, unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 13 mwezi 05 mwaka 2022 saa 2 Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea. Angalizo: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 mwezi wa 04 mwaka 2022.**

..............................
**HAKIMU**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

TEDDY FULGENCE MSAKI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA COROLLA RANX yenye namba za usajili T 225 DCN,yeyote atakayeiokot atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa ARU/ARU/RB/173386/2022

## TANGAZO KUPOTEA NYARAKA YA UMILIKI WA KIWANJA

Joseph Bunango Chagula anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 42 kitalu "RR" kilichopo Bushushu Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilichopo Karibu au awasiliane na Joseph Bunango Chagula kwa simu namba 0786-504005

Rbnamba /SHI/SHI/RB/172368/2022

Pokea nyaraka za tangazo na slip ya malipo ya Tangazo

Jacob F.Mwinuka
AFISA ARDHI
MANISPAA YA SHINYANGA
hi wa Habari- Shinyanga
AFISA ARDHI WA MANISPAA SHINYANGA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

HAMAD KHAMIS MSELLEM anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA HIACE yenye namba za usajili T 591 AYZ ,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa ARU/ARU/RB/162587/2022

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mume aua mke kisa chumvi nyingi

**Mumbai,** INDIA

POLISI nchini India walimkamata mwanaume mwenye umri wa miaka 46 ambaye anadaiwa kumuua mkewe kwa sababu kifungua kinywa chake kilikuwa na chumvi nyingi.

"Nikesh Ghag, karani wa benki huko Thane, karibu na mji wa magharibi wa Mumbai, alimnyonga mke wake mwenye umri wa miaka 40 kwa hasira kwa sababu chakula kinachofahamika kama khichdi ya sabudana [tapioca lulu au sago] alichokuwa anamwandalia kilikuwa na chumvi nyingi,"ofisa wa polisi Milind Desai, amesema.

Mtoto wa wanandoa hao mwenye umri wa miaka 12, ambaye alishuhudia uhalifu huo, aliwaambia polisi kwamba baba yake alimfuata mama yake, Nirmala, chumbani akilalamikia chumvi iliyopitiliza kwenye chakula na kuanza kumpiga.

"Aliendelea kulia na kumwomba aache anachofanya," Desai alisema, "lakini mshtakiwa aliendelea kumpiga mkewe na kumnyonga kwa kamba".

Ghag alitoka nje ya nyumba kwa nguvu, mtoto huyo aliwaita bibi yake mzaa mama na mjomba wake.

"Kufika eneo la tukio, familia yake ilikuwa imemkimbiza hospitalini, lakini wakati huo alikuwa tayari amefariki," Desai alisema.

Baadaye mshtakiwa alijisalimisha katika kituo cha polisi, aliwaambia maofisa kuwa anasumbuliwa na shinikizo la damu.

**ALIPELEKWA JELA**

Familia ya Nirmala iliiambia polisi kwamba Ghag amekuwa akizozana naye kuhusu masuala ya nyumbani kwa siku 15 zilizopita.

Desai alisema hawajapokea malalamishi yoyote kuhusu hili kutoka kwa mwathiriwa au familia yake.

Mauaji ya mwanamke na mumewe, yaliyochochewa na ugomvi juu ya chakula, mara kwa mara yanagonga vichwa vya habari nchini India.

Matukio mengi yakiripotiwa chini ya kisheria ya ukatili wa mume au jamaa zake, unyanyasaji wa nyumbani mara kwa mara umekuwa uhalifu wa kikatili dhidi ya wanawake unaoripotiwa zaidi nchini India mwaka baada ya mwaka. **BBC**

# OPEC wakutana leo kujadili kupaa bei ya mafuta duniani

**Vienna,** AUSTRIA

WAZALISHAJI wakubwa wa mafuta duniani wanakutana leo, huku kukiwa na wito kutoka kote duniani kushinikiza bei ya bidhaa hiyo kupunguzwa.

Wanachama wa kundi la wazalishaji wa mafuta la Opec, ambalo linajumuisha Russia, hawana haraka ya kufanya hivyo.

Opec+ ni kundi la nchi 23 zinazouza nje mafuta ambazo hukutana kila mwezi mjini Vienna, kuamua ni kiasi gani cha mafuta ghafi kinafaa kuweka kwenye soko la dunia.

Kundi hilo linajumuisha nchi 13 wanachama wa Opec, ambazo ni pamoja na nchi za Mashariki ya Kati na Afrika.

Lilianzishwa mwaka wa 1960 kama chombo maalum, kwa lengo la kudhibiti usambazaji wa mafuta na bei yake kote duniani.

Opec huzalisha asilimia 30 ya mafuta ghafi duniani, takriban mapipa milioni 28 kwa siku.

Mzalishaji mkubwa wa mafuta ndani ya Opec ni Saudi Arabia, ambayo inazalisha zaidi ya mapipa milioni 10 kwa siku.

Mwaka 2016, wakati bei ya mafuta ilikuwa chini, OPEC iliungana na wazalishaji 10 wa mafuta wasio wa Opec kuunda Opec+.

**Juni mwaka 2021, huku mahitaji ya mafuta ghafi yakianza kupata nafuu, Opec+ ilianza kuongeza usambazaji polepole na kuweka mapipa 400,000 zaidi kwa siku kwenye masoko ya dunia.**

Miongoni mwao ni Russia, ambayo pia inazalisha zaidi ya mapipa milioni 10 kwa siku. Kwa pamoja nchi hizo zinazalisha karibu asilimia 40 ya mafuta yote ghafi duniani.

"Watengenezaji mafuta wa Opec+ wanasambaza mahitaji ya kusawazisha soko," anasema Kate Dourian wa Taasisi ya Nishati, akiongeza:

"Wanaweka bei juu kwa kupunguza usambazaji wakati mahitaji ya mafuta yanapungua."

Opec+ pia inaweza kupunguza bei kwa kuweka mafuta zaidi kwenye soko jambo ambalo waagizaji wakubwa kama vile Marekani na Uingereza wanataka ifanye.

Mwaka 2020, wakati wa Uviko-19 ilipoenea duniani nchi ziliweka amri ya kutotoka nje, bei ya mafuta ghafi ilianguka kwa sababu ya ukosefu wa wanunuzi.

"Wazalishaji walikuwa wakiwalipa watu kuchukua mafuta kutoka kwa mikono yao, kwa sababu hawakuwa na nafasi ya kutosha ya kuhifadhi yote," anasema Dourian.

Baada ya hayo, wanachama wa Opec+ walikubali kupunguza uzalishaji kwa mapipa milioni 10 kwa siku, ili kuongeza bei.

Juni mwaka 2021, huku mahitaji ya mafuta ghafi yakianza kupata nafuu, Opec+ ilianza kuongeza usambazaji polepole na kuweka mapipa 400,000 zaidi kwa siku kwenye masoko ya dunia.

Sasa inasambaza mapipa milioni 2.5 ya mafuta kwa siku chini ya msimu wa joto na baridi wa 2020.

Hata hivyo, Russia ilipovamia Ukraine, bei ya mafuta ghafi ilipanda hadi zaidi ya dola 100 kwa pipa.

Hiyo imesababisha kupanda kwa kiasi kikubwa kwa bei ya petroli katika vituo vya kuuza mafuta.

"Wakati Opec+ ilipopunguza uzalishaji kwa pipa milioni 10 kwa siku mnamo mwezi Mei 2020, walipunguza sana," anasema David Fyfe, Mchumi Mkuu katika taasisi ya Argus Media.

"Sasa wanaongeza usambazaji kwa kasi ndogo ambayo haizingatii athari za mzozo wa Urusi na Ukraine."

Kuna wasiwasi miongoni mwa wanunuaji mafuta kwamba Umoja wa Ulaya (EU) utafuata mkondo wa Marekani na kuweka vikwazo vya kuagiza mafuta kutoka Russia, anasema Fyfe. **BBC**

UCHAGUZI MKUU KENYA 2022:

# Raila: Nitawapeleka kwenye uchumi imara

**Nairobi,** KENYA



KIONGOZI wa Narc-Kenya, Martha Karua alikuwa na wakati mgumu kutuliza umati uliojitokeza kumsikiliza kiongozi wa Chama cha ODM, Raila Odinga (pichani) eneo la Kutus, Kirinyaga.

Raila alizuru eneo hilo juzi, kutafuta uungwaji mkono katika uchaguzi mkuu Agosti 9, mwaka huu, akilenga kumrithi Rais Uhuru Kenyatta.

Ilichukua muda kwa Karua kutuliza umati uliomzomea.

"Sisi hatutaki watu wa kuharibu wengine mikutano yao. Ninawaomba mheshimu baba (akimaanisha Raila Odinga).

Waliolipwa kuja kuharibu mkutano wa baba, hatutakubali. Waandae mikutano yao hatutaihudhuria," Karua alisema, akiwataka maofisa wa polisi kusaidia kutuliza waliotaka kuzua fujo.

Licha ya mtafaruku huo wa Kutus, Raila alihutubia waliojitokeza wakimshangilia alivyouza sera zake.

"Mwaka huu ni wa ukombozi wa tatu. Ukombozi wa kwanza ulikuwa wa uhuru, wa pili Katiba, na wa tatu ni wa kiuchumi," Waziri Mkuu huyo wa zamani alielezea.

Vilevile, alisisitiza lengo lake ni kupambana na maadui watatu: Ugonjwa, ujinga na maskini.

Chini ya muungano wa Azimio One Kenya, Raila pia alikuwa ameandamana na gavana wa Laikipia, Nderitu Muriithi, mbunge mwakilishi wa wanawake Murang'a, Sabina Chege, Naibu Gavana Nyeri, Caroline Karugu, miongoni mwa viongozi na wanasiasa wengine wanaompigia debe.

"Ukiona mtu analeta fujo kwenye mkutano wa mtu mwingine, hana sera wala ajenda," Muriithi alisema, akikashifu waliomzomea Karua.

Juzi, ilikuwa siku ya pili Raila kutafuta uungwaji mkono Mlima Kenya, Jumapili akijikita kambi Nyeri.

Pia, Jumamosi wiki iliyopita, aliungana na Rais Kenyatta katika mazishi ya Rais wa tatu wa Kenya, Mzee Mwai Kibaki aliyezikwa nyumbani kwake Othaya, Nyeri.

Naibu Rais William Ruto ambaye anasaka kura kuingia Ikulu, amekuwa akidai eneo la Kati ni ngome yake ambako anasema ana ufuasi mkubwa Mlima Kenya. **TAIFA LEO**

# KANGWA AKIRI MSIMU MGUMU KWA AZAM FC

**Na Saada Akida**

BEKI wa Azam FC, Bluce Kangwa, amekiri msimu huu haukuwa mzuri kwao kutokana na kushindwa kutimiza malengo ya mbio za ubingwa, hivyo sasa wanapambana kutafuta nafasi tatu za juu katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyobaki.

Azam FC juzi waliambulia suluhu dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Kaitaba mkoani Kagera, iliyowafanya 'Wanalambalamba' hao kusalia katika nafasi ya nne ikiwa na pointi 29 katika msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kangwe alisema hawakuwa na msimu nzuri katika kuhakikisha wanafikia yale waliyodhamiria mwanzoni mwa msimu, hivyo sasa wanapigania kutafuta pointi muhimu katika michezo yao ili kuhakikisha hawatoki katika tatu bora kwenye msimamo.

Alisema mechi yao dhidi ya Kagera Sugar ilikuwa ngumu na ushindani mkubwa kama ilivyo ligi, kwa hiyo wanajipanga kuhakikisha wanapambana kutafuta matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao.

"Tumemaliza mechi dhidi ya Kagera Sugar kwa kupata pointi moja na sasa tunarejea Dar es Salaam kujiandaa na michezo iliyopo mbele yetu ikiwamo dhidi ya KMC FC tutakaocheza hivi karibuni," alisema Kangwa.

Alisema hakuna mechi iliyorahisi, lakini watajipanga kwa mchezo ujao na ana imani kocha wao, Abdihamid Moallin atafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo uliopita wakati wakijiandaa na mechi ijayo.

Azam FC watashuka dimbani Mei 7, dhidi ya KMC FC katika mchezo utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex na Mei 10, mwaka huu, watakuwa ugenini dhidi ya Mbeya City katika dimba la Sokoine jijini Mbeya.

## *Serengeti Girls yaanza kuiwinda Cameroon*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17, Serengeti Girls, imeanza maandalizi kabambe kuivaa timu ya Taifa ya Cameroon kwenye mechi ya mwisho ya mchujo, kwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia zinazotarajiwa kufanyika, Oktoba 11 hadi 30, mwaka huu nchini India.

Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Oscar Milambo, amesema baada ya mechi dhidi ya Burundi, timu hiyo imeingia kambini moja kwa moja bila kupumzika ili kupata muda mrefu wa kujiandaa kutokana na aina ya mpinzani ambaye wanakwenda kukutana naye.

"Timu haitokuwa na mapumziko, Cameroon tunaifahamu, ni tofauti na sisi, ni timu kubwa tofauti na sisi kama nchi kwenye mpira wa wanawake, ushindani utakuwa mkubwa, na tunafahamu, hivyo tunapaswa kujiandaa kuona tutacheza na taifa kubwa, siyo kupiga hatua, lakini kushinda na kwenda kwenye fainali za Kombe la Dunia," alisema Milambo.

Timu ya Serengeti Girls iliingia kwenye hatua ya pili ya mchujo, baada ya kuiondosha kwenye mashindano timu ya Taifa ya Burundi kwa jumla ya mabao 5-2.

Kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa mwezi uliopita nchini Burundi, Tanzania ikishinda mabao 4-1, lakini mchezo wa marudiano hivi wiki iliyopita katika Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar, timu hiyo ilipoteza kwa mabao 2-1, matokeo ambayo hayakuathiri nafasi yao ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Kama Serengeti Girls itapata matokeo ya jumla dhidi ya Cameroon katika mechi mbili ya nyumbani na ugenini, itakuwa imefuzu moja kwa moja na kutinga kwenye fainali hizo kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi, ambazo zitafanyika nchini India Oktoba mwaka huu.

## SOKA LIENDELEE...




Meneja Mkuu wa Kampuni ya Refuelling Solutions (T) Ltd (RSTL), Renatus Mabeyo (kulia), akikabidhi jezi 34 za mchezo wa soka, kwa Mwenyekiti wa Vijana CCM Bwawani Kata ya Kijitonyama wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, Twaha John, ikiwa ni sehemu ya kampuni hiyo kushiriki shughuli mbambali za kijamii, kiuchumi, pamoja na michezo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Kichuya: Naijua vizuri Simba SC, hainisumbui

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Namungo FC, Shiza Kichuya, amesema huwa hapanii akicheza mechi dhidi ya Simba, bali huwa anawafahamu vizuri mabeki wa timu hiyo kwa sababu amewahi kucheza na baadhi yao katika kikosi hicho.

Kichuya alisema hayo baada ya mechi ya Ligi Kuu kati ya timu yake ya Namungo na Simba iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi na timu hizo kutoka sare ya kufungana mabao 2-2.

"Sijapania mechi, wala hakuna mchezaji wa Namungo aliyepania, tumecheza kutokana na maelekezo ya walimu wetu walivyotuagiza. Unajua mimi na Tshabalala ni marafiki tangu tuko Simba kwa hiyo tunajuana, yeye ananijua na mimi namjua yeye, tunapokutana inakuwa ni balaa, kila mtu anataka kumwonyesha mwenzake kazi, mechi ikiisha tunabaki kuwa marafiki.

"Unajua kumpita beki kila mtu ana mbinu zake, ndiyo maana unaona leo nilikuwa nampita na yeye pia alikuwa anapanda hadi inabidi na mimi niende kumkaba. Tunapambana kweli, ila leo mimi nimemshinda," alisema.

**Alisema kuwa si kwa Tshabalala tu, bali hata baadhi ya mabeki wa Simba hawampi tabu sana kwa sababu ameshacheza nao wakiwa timu hiyo.**

Kwenye mechi hiyo, Kichuya alisema kuwa anashangaa kuona watu wanawafanya kama vile wameshinda kutokana na kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Simba, wakati na wao kuna kitu wamekikosa kwani walikuwa wanahitaji ushindi.

"Siyo Simba wamepoteza, hata sisi tumepoteza, sisi pia tulihitaji pointi tatu ili tukae sehemu nzuri, lakini imeshindikana, timu zote zimepoteza kwa kupata pointi moja," alisema Kichuya.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LUKAKU HAENDI MILAN
MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku hana nia ya kujiunga na AC Milan ama Newcastle msimu huu wa majira ya joto, licha ya mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 28 kukosa nafasi ya kucheza pale Chelsea. (***Evening Standard***)

### DE JONG FEDHA NDEFU
BARCELONA itapokea fedha nyingi kwa ajili ya kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong. Manchester United wamehusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, huku Erik ten Hag, ambaye alikuwa akimfundisha De Jong katika Klabu ya Ajax, akichukua mikoba kama kocha wa Old Trafford msimu huu wa majira ya joto. (***Sport***)

### TEN HAG KUSAJILI BEKI
KOCHA Erik ten Hag, amebainisha wachezaji wanane ambao anaweza kuwategemea atakapoanza kazi Manchester United. Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 52, ana matumaini ya kumsajili beki wa kushoto na kati kumsaidia Harry Maguire mwenye miaka 29. (Telegraph)

### NUNEZ AWANIWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle imekuwa ikitaka kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Benfica na Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22, ambaye amehusishwa na uhamisho wa kwenda Manchester United na Liverpool. (***Mirror***)

### CONTE KUIJENGA SPURS
KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte anapania kuimarisha kikosi chake msimu huu wa majira joto kwa kuwasajili kiungo wa kati wa Southampton na England, James Ward-Prowse mwenye umri wa miaka 27. (***Fichajes***)

### COUTINHO NA HATIMA
ASTON Villa wameambiwa na Barcelona kwamba wana hadi mwisho wa Mei kuamua ikiwa wanataka kumsajili kiungo wa Brazil, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 29, kwa mkataba wa kudumu msimu huu wa majira ya joto. (***Sport***)

### GVARDIOL AWANIWA CHELSEA
CHELSEA wanataka kumsajili mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 20, kutoka RB Leipzig huku, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 29 na Andreas Christensen, 26, akitarajia kujiunga na Real Madrid au Barcelona. (***Goal***)

### INTER KUMUUZA DE VRIJ
INTER Milan inataka kumuuza Stefan de Vrij kwa pauni milioni 15 msimu huu wa majira ya joto, huku Tottenham, Aston Villa na Newcastle zikiwa miongoni mwa klabu zinazomhitaji mlinzi huyo wa kati wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 30. (***Football Insider***)

### UNITED YAMSHINDWA ADEYEMI
KLABU ya Manchester United imeshindwa katika jaribio lao la kumsajili mshambuliaji Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 20. (***Patrick Berger***)

### GOMEZ ATAKIWA FULHAM
KLABU ya Fulham iliyopanda daraja inaweza kumsajili beki wa Liverpool, Joe Gomez mwenye umri wa miaka 24. (***Football League World***)

### NKETIAH KUONGEZEWA MKATABA
ARSENAL itafanya jaribio la mwisho la kumpa mkataba mpya mshambuliaji wa England, Eddie Nketiah. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa Juni, anasakwa na klabu kadhaa za England, Ufaransa na Ujerumani. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH: NAIOGOPA MAN CITY KULIKO REAL MADRID

●●● Kwa sababu tulipoteza katika fainali dhidi ya Real, lazima niseme ukweli City ni timu ngumu sana, tulicheza...

**LIVERPOOL,** ENGLAND

MOHAMED Salah angependa kukutana na Real Madrid kuliko Manchester City kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kule Paris, huku akilenga kubeba mataji manne msimu huu baada ya ushindi dhidi ya Villarreal, Jumanne.

Liverpool walitinga fainali yao ya 10 ya Ulaya, huku Fabinho, Luis Diaz, na Sadio Mane wakifunga mabao ya kipindi cha pili baada ya Villarreal kuongoza kipindi cha kwanza.

Liverpool imekuwa timu ya kwanza kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la FA, na Kombe la Ligi katika msimu mmoja, na imepitwa pointi moja na Man City kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England.

"Ndio, (ni lengo) kwa hakika," alisema akiiambia BT Sport.

"Labda si mwanzoni mwa msimu ikiwa ninasema ukweli, kwa sababu huwa nazingatia Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu, lakini sasa tuko karibu kwa kila kitu, kwa nini sivyo?

"Nadhani baada ya kuifunga City katika nusu fainali ya Kombe la FA (Liverpool waliamini kuwa inawezekana), lakini kwenye Ligi ya Mabingwa, tangu mwanzo tulikuwa tunacheza michezo ya ajabu, tulikuwa na kundi gumu sana na tulishinda.

"Kwa hiyo nilisema kutoka wakati huo tunaweza kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka huu.

"Nataka kucheza na Madrid, lazima niseme ukweli. City ni timu ngumu sana, tulicheza dhidi yao mara chache msimu huu, lakini nadhani ukiniuliza mimi binafsi, ningeipendelea Madrid.

"Kwa sababu tulipoteza katika fainali dhidi yao, nataka kucheza dhidi yao, na ninatumaini kushinda dhidi yao pia."

Salah alisaidia bao muhimu la Fabinho dakika ya 62 na kufikisha mabao 45 katika michuano yote msimu huu (mabao 30, asisti 15), na mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri alifichua kuwa alikuwa amejiwekea lengo la kufunga mabao 40 kabla ya msimu kuanza.

"Ninaipa timu kila kitu, lazima tujikite kwenye timu kwa sababu tunapambana kwa kila kitu, tumeshinda kombe moja tayari, tuko kwenye fainali, tunaendelea kupigania Ligi Kuu na tuko fainali dhidi ya Chelsea (katika Kombe la FA)," aliongeza.

"Ninazingatia tu, na kujaribu kufanya mazoezi kwa bidii. Ninajua ninachotaka mwishoni mwa msimu, kwa hiyo ninatumaini naweza kupata kile ninachotaka."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,224

MECHI KALI
BIASHARA UNITED
VERSUS
DODOMA FC
1 | 1.86
X | 2.92
2 | 4.57

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MULLER AONGEZA MKATABA BAYERN



**MUNICH,** Ujerumani

THOMAS Muller ameongeza mkataba wake na Bayern Munich hadi mwishoni mwa msimu wa 2023-24, mabingwa hao wa Bundesliga wametangaza.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, ambaye ametumia muda wake wote wa uchezaji kwa misimu 14 akiwa na Bayern, mkataba wake ulikuwa unamalizika mwishoni mwa msimu ujao.


Hata hivyo, baada ya kuwa mchezaji muhimu wakati wakitwaa taji la 10 mfululizo la ligi msimu huu, Muller na Bayern wamekubaliana katika masharti mapya.

"Nimefurahi kuongeza mkataba wangu na FC Bayern Munich hadi 2024," alisema Muller akiiambia tovuti rasmi ya klabu hiyo Jumanne wiki hii.

"Safari ambayo tumekuwa nayo tangu nilipojiunga na akademi ya FCB mwaka 2000 imekuwa hadithi nzuri ya mafanikio hadi sasa.

Muller ameshinda mataji 11 ya Bundesliga akiwa na Bayern, huku ushindi wake wa msimu huu umemfanya kumpita David Alaba (10) kama mchezaji aliyebeba mataji mengi zaidi ya ligi hiyo.

Amecheza mechi 624 katika kikosi cha kwanza na pia amebeba Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili, Kombe la Klabu Bingwa Dunia, UEFA Super na mataji sita ya DFB-Pokal.



# Rangnick na matarajio ya Ronaldo kubaki Utd

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo bado atakuwa Manchester United msimu ujao, kwa mujibu wa kocha anayeondoka, Ralf Rangnick.

Mabadiliko makubwa yanatarajiwa katika Uwanja wa Old Trafford katika msimu ujao huku kocha mpya Erik ten Hag akichukua nafasi ya Rangnick, ambaye anachukua nafasi mbili kama mshauri wa United na kocha wa Austria.

Nemanja Matic, Juan Mata na Edinson Cavani wote walicheza mechi zao za mwisho nyumbani kama wachezaji wa United katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Brentford, Jumatatu.

Na pia kumekuwa na uvumi mwingi kuhusu Ronaldo na jinsi atakavyofanya chini ya Ten Hag - au kama anaweza hata kuhama mwaka mmoja baada ya kurejea klabuni hapo.

Lakini Ronaldo amefunga mabao 18 katika mechi 29 za Ligi Kuu msimu huu, na Rangnick haoni kwamba nyota huyo ataondoka United.

Akizungumza na BT Sport, baada ya mechi dhidi ya Brentford, kuhusu Ronaldo, Rangnick alisema: "Sidhani kama ataondoka.

HABARI MICHEZO

4,601,040

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/05/22 | 17:00 | Burnley vs Aston Villa | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 02. 07/05/22 | 17:00 | Brentford vs Southampton | 2.21 | 3.37 | 3.02 |
| 03. 07/05/22 | 19:00 | Sassuolo vs Udinese | 2.25 | 3.56 | 2.82 |
| 04. 07/05/22 | 19:30 | Brighton vs Manchester Utd | 2.62 | 3.21 | 2.58 |
| 05. 07/05/22 | 19:30 | Hertha BSC vs Mainz | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 06. 07/05/22 | 20:00 | Benfica vs Porto | 2.74 | 3.43 | 2.39 |
| 07. 08/05/22 | 16:00 | Leicester vs Everton | 2.31 | 3.22 | 2.97 |
| 08. 08/05/22 | 16:00 | Venezia vs Bologna | 2.93 | 3.27 | 2.31 |
| 09. 08/05/22 | 17:15 | Villarreal vs Sevilla FC | 2.30 | 3.25 | 3.05 |
| 10. 08/05/22 | 17:45 | Feyenoord vs PSV Eindhoven | 2.41 | 3.62 | 2.58 |
| 11. 08/05/22 | 19:00 | Salernitana vs Cagliari | 2.35 | 3.26 | 2.87 |
| 12. 08/05/22 | 19:30 | Espanyol vs Osasuna | 2.59 | 3.14 | 2.74 |
| 13. 08/05/22 | 22:00 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.37 | 3.30 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 05/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5057 | Mbeya Kwanza FC vs Tanzania Prisons | 2.35 | 2.70 | 3.65 |
| 15:00 | 2189 | Bkma Yerevan vs Van Yerevan | 3.41 | 2.97 | 2.13 |
| 15:30 | 1806 | Baia Zugdidi vs Gareji | 3.06 | 3.55 | 2.03 |
| 15:30 | 3864 | Metalurgi R vs Merani Martvili | 3.44 | 3.40 | 1.94 |
| 15:30 | 5652 | FC Spaeri vs FC Norchi Dinamo Tbilisi | 3.90 | 3.70 | 1.74 |
| 16:00 | 2908 | KF Ballkani vs Malisheva | 1.42 | 4.40 | 7.20 |
| 16:00 | 3684 | FC Zvezda Perm vs Dinamo Barnaul | 1.46 | 4.50 | 6.20 |
| 16:00 | 4076 | Al-Bourj FC vs AL Ahed | 3.54 | 3.01 | 2.06 |
| 16:00 | 4199 | KF Drenica Skenderaj vs KF Llapi | 2.01 | 3.61 | 3.07 |
| 16:00 | 4843 | Biashara United vs Dodoma FC | 1.86 | 2.92 | 4.57 |
| 16:30 | 4687 | FC Olimpik vs Dinamo Samarqand | 2.40 | 2.63 | 3.31 |
| 16:30 | 5960 | Neftchi Fargona vs Lokomotiv Tashkent | 3.21 | 2.92 | 2.24 |
| 17:00 | 2612 | Emirates Club vs Baniyas | 3.80 | 3.66 | 1.77 |
| 17:00 | 3849 | FK Tyumen vs Irtysh | 1.38 | 5.20 | 6.60 |
| 17:00 | 4751 | AL Khaleej Khor Fakkan vs AL Urooba | 1.42 | 4.55 | 5.62 |
| 17:30 | 1162 | Shams Azar Qazvin vs Shahin Bushehr | 1.38 | 3.91 | 8.41 |
| 17:30 | 1482 | Saipa Karadj vs Esteghlal Mollasani | 2.07 | 2.95 | 4.00 |
| 17:30 | 2997 | Khosheh Talaei vs Malavan Bandar Anzali | 5.05 | 2.22 | 2.21 |
| 17:30 | 4072 | Mes Shahr-e Babak vs Arman Gohar Sirjan | 3.55 | 2.53 | 2.37 |
| 17:30 | 4401 | BFC Daugavpils vs Rigas Futbola Skola | 9.75 | 5.27 | 1.24 |
| 17:30 | 4661 | Shahrdari Astara vs Rayka Babol | 2.21 | 2.85 | 3.75 |
| 17:30 | 4739 | Sanat Mes Kerman FC vs Ghasghaei Shiraz | 1.46 | 3.85 | 8.00 |
| 17:45 | 1564 | Din. Tirana vs Vllaznia | 3.85 | 2.88 | 2.03 |
| 18:00 | 1990 | Spartaks Jurmala vs Valmiera Fk/Bjss | 12.63 | 5.64 | 1.19 |
| 18:00 | 5819 | Pars Jonoubi Jam vs Machine Sazi Tabriz | 1.32 | 4.17 | 9.71 |
| 18:30 | 3941 | Pyunik Yerevan vs Artsakh | 1.62 | 3.44 | 5.23 |
| 18:50 | 5180 | Hajer Club vs Al Khaleej Club | 2.62 | 2.76 | 2.81 |
| 19:00 | 1857 | Kisvarda FC vs Ujpest FC | 2.04 | 3.31 | 3.26 |
| 19:00 | 2650 | Salernitana vs Venezia | 1.77 | 3.62 | 4.16 |
| 19:00 | 3648 | Odense vs Sonderjyske | 1.82 | 3.65 | 3.60 |
| 19:00 | 5849 | AL Kawkab vs Al Jabalain | 4.20 | 3.00 | 2.02 |
| 19:05 | 5384 | AL Draih vs Ohud Medina | 3.60 | 3.00 | 2.19 |
| 19:20 | 2192 | Al Taawon vs Al-Ettifaq | 2.04 | 3.30 | 3.60 |
| 19:45 | 1449 | Al Nasr Dubai vs Al Wasl Dubai | 2.17 | 3.60 | 2.77 |
| 20:00 | 2031 | Hedensted IF vs OKS | 2.52 | 3.69 | 2.31 |
| 20:00 | 2811 | Hermanstadt vs Petrolul Ploiesti | 2.24 | 2.97 | 3.16 |
| 20:00 | 3378 | Hammer Spvg vs Holzwickeder SC | 1.99 | 3.85 | 2.97 |
| 20:00 | 4149 | Djurgardens IF vs Helsingborg | 1.40 | 4.29 | 6.44 |
| 20:30 | 1580 | TUS Ennepetal vs TSG Sprockhovel | 2.97 | 3.85 | 1.99 |
| 20:30 | 2404 | Najran SC vs AL Akhdood | 2.12 | 2.92 | 3.50 |
| 20:30 | 3946 | FC Gutersloh vs Siegen | 1.38 | 4.69 | 6.25 |
| 20:45 | 5615 | SC Preussen Munster II vs SG Finnentrop | 2.05 | 3.80 | 2.87 |
| 20:50 | 3834 | Jeddah Club vs Al Wehda | 3.69 | 2.86 | 2.09 |
| 20:50 | 5746 | AL Baten vs Al Ahli Jeddah | 3.40 | 3.50 | 2.04 |
| 21:45 | 3496 | Wycombe vs MK Dons | 2.46 | 3.13 | 2.83 |
| 22:00 | 2172 | Marseille vs Feyenoord | 2.13 | 3.69 | 3.04 |
| 22:00 | 4870 | Roma vs Leicester | 2.13 | 3.30 | 3.35 |
| 22:00 | 5053 | Rangers vs RB Leipzig | 3.40 | 3.50 | 2.04 |
| 22:00 | 5423 | Eintracht Frankfurt vs West Ham | 2.47 | 3.40 | 2.70 |
| 23:00 | 1480 | CD Cortulua vs CD La Equidad | 2.22 | 3.01 | 3.15 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# KOCHA JULIO AANIKA UDHAIFU WA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Simba, juzi kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amewachambua wapinzani wao hao na kuwaeleza makosa wanayotakiwa kuyafanyia kazi mapema ambayo yamekuwa yakitumiwa na timu pinzani kuwaadhibu.

**Akizungumzia mchezo huo na matokeo waliyoyapata, Julio, alisema awali aliwaambia watu kuwa hawezi kufungwa na Simba, na kweli imetokea.**

"Niliwaambia watu kuwa siwezi kufungwa na Yanga, lakini tukafungwa kwa sababu ya makosa ya mabeki wangu, na nikasema siwezi kufungwa na Simba, na kweli tulikuwa tunashinda hii mechi kama si makosa ya mabeki wangu pia," alisema Julio.

Hata hivyo, aliitahadharisha Simba kuwa ilifanyie kazi suala la kuruhusu kufungwa mabao ya faulo, kona, krosi na mipira ya juu kirahisi.

"Simba ina matatizo ya kufungwa mabao yanayotokana na mipira ya kona, krosi, faulo na ile ya juu, wamefungwa mabao kirahisi na kizembe ambayo kwa timu kubwa hawakutakiwa kufungwa, inafaa walifanyie kazi kama watakwenda tena kimataifa," alisema Julio.

Takwimu zinaonyesha Simba imeruhusu mabao matano ya mipira ya juu kati ya tisa ya Ligi Kuu msimu huu.

Pia imekuwa ikifungwa aina hiyo ya mabao kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho msimu huu, kwani hata bao la Orlando Pirates kwenye mechi iliyochezwa nchini Afrika Kusini lilikuwa la aina hiyo.

Kwa upande wa Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally amesema kuwa japo matumaini ya ubingwa ni hafifu kwao, lakini wataendelea kupambana ili kutowavunja nguvu na kuwakatisha tamaa mashabiki wao ambao huwa wanajitokeza kwa wingi viwanjani kwenda kuishangilia.

"Ni kweli hatuko kwenye nafasi nzuri, lakini bado tuna mechi tisa mkononi na tunaendelea kupambana, ukikata tamaa unawavunja morali hata mashabiki wetu wanaokuja kwenye viwanja. Sisi kama Simba tutaendelea kucheza kwa nguvu na morali ule ule ili kuhakikisha tunapata matokeo, mfano tuna mechi huko Geita, tunakwenda kucheza na Geita Gold, hatujafika huko muda mrefu, mashabiki wanatusubiria kwa hamu, hivi leo uache upuuzie kwa sababu tu hatuna matumaini ya ubingwa, inakuwa ni kuwanyong'onyesha.

"Kwa hiyo sisi Simba kama timu kubwa pamoja na kwamba matumaini ni madogo, lakini tutahakikisha tunapambana kila mchezo," alisema Meneja huyo.

Akizungumzia mechi hiyo, alisema kuwa Namungo FC walikuwa bora na walipata bahati ya kuwatangulia mara mbili, lakini wachezaji wao walipambana na kurudisha mabao.

"Si matokeo ambayo tunayataka, hayatufurahishi, tulitaka tushinde mechi zote bila kuangalia timu nyingine inafanya nini, lakini ni matokeo ya mchezo lazima yaheshimiwe," alisema.

Pamoja na sare hiyo, bado Simba imeendelea kuhodhi nafasi ya pili ikiwa na pointi 43, huku Namungo ikiwa kwenye nafasi yake ya tatu kwa pointi 30.



Mshambuliaji wa Simba, Denis Kibu, akiifungia timu yake bao la kusawazisha wakati ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Namungo kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi juzi. **PICHA: SIMBA**

# *Mtibwa yachekelea sare Biashara ikinuna*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mtibwa Sugar imesema imefurahishwa na sare ya bao 1-1 iliyoipata dhidi ya Biashara United kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza ikidai kuwa itawasaidia baadaye kwenye harakati za kuwaepusha kushuka daraja.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Awadh Juma, amesema pointi hiyo ambayo wameipata ugenini, imewafanya wapate nguvu ya kupambana zaidi kuiondoa timu yao kwenye eneo la hatari.

"Tunashukuru Mungu, tumegawana pointi na Biashara, siyo kazi rahisi kwa sababu tulikuwa ugenini na Biashara United ni timu nzuri sana," alisema Awadh.

Wakati Mtibwa ikichekelea sare hiyo, Kocha Mkuu wa Biashara United, ameonyesha kukasirishwa, akisema kuwa wachezaji wake wamefanya uzembe kuwaachia wapinzani wao wamiliki mpira dakika za mwisho.

"Tumewaachia wamiliki mpira dakika 10 za mwisho, wakatufunga, huwezi kuwaruhusu wapinzani wawe na mpira muda wote, wakiwa wanapiga krosi nyingi, watakufunga tu. Hilo ndilo tatizo, lakini mechi tulikuwa tumeimaliza kwa sababu wamerudisha dakika ya 90," alisema Bahati raia wa Burundi.

Mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyochezwa Jumatatu wiki hii kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, Mpapi Nassibu akiipatia Biashara United bao dakika ya 44, kabla ya Nzigamasabo Styve kuisawazisha Mtibwa Sugar dakika ya 90.

# Michezo

Alhamisi Mei 5, 2022

Nipashe




## Salah: Naiogopa Man City kuliko Real Madrid

HAPO MWISHO...



Kiungo mkabaji wa Ruvu Shooting, Ally Kombo, akimdhibiti mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, kuliona lango lao huku Nathaniel Chilambo (kulia), akiwahi kwenda kutoa msaada kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma na kumalizika kwa sare tasa jana. **PICHA: YANGA**

## Pablo awashukia mabeki Simba

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amekuwa mkali kwa safu yake ya ulinzi kwa kuieleza kwamba haitakiwi kufanya makosa kama waliyofanya juzi dhidi ya Namungo FC, hali ambayo inawaweka katika wakati mgumu zaidi kwenye vita vya mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba wakiwa ugenini juzi walilazimisha sare ya mabao 2-2 dhidi ya Namungo FC katika mchezo wa ligi hiyo uliopigwa kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi hivyo kurejea Dar es Salaam wakiwa na pointi moja baada kukamilika kwa dakika 90 za mchezo huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pablo alisema walifanya makosa ya kiulinzi yaliyoifanya Namungo kupata mabao mepesi katika mchezo huo uliomalizika kwa sare ya 2-2.

Alisema Simba ni timu kubwa inayopambania kutetea ubingwa, hivyo hawatakiwi kufanya makosa kama waliyofanya dhidi ya Namungo na kuwaweka katika mazingira magumu.

"Mbali na safu ya ulinzi, kwa timu kubwa kufanya makosa ya ulinzi haileti picha nzuri na pia tumetengeneza nafasi ambazo hatukuzitumia vizuri.

"Safu ya ushambuliaji hawakuwa vizuri katika kumalizia nafasi walizopata hasa kipindi cha kwanza katika mchezo huu uliokuwa wa ushindani na mzuri kwa kila timu," alisema Pablo.

Alisema wanarudi nyumbani kuendelea kujipanga kwa mchezo unaofuata kuhakikisha wanapambana kutafuta pointi muhimu katika michezo iliyoko mbele yao kufikia malengo yao ya kutetea ubingwa.

"Tunarudi kuendelea kujipanga kwa mchezo unaofuata, bado hutujakata tamaa katika mbio za ubingwa na tutahakikisha tunapambana kupata alama tatu kwenye kila mechi uliopo mbele yetu," alisema kocha huyo.

Kikosi cha Simba kilirejea Dar es Salaam jana, Jumatano, kuendelea kujipanga kwa mchezo ujao dhidi ya Ruvu Shooting utakaopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

# YANGA YAPUNGUZWA KASI YA UBINGWA

## ●●●Ruvu Shooting yaibana koo Kigoma mwanzo mwisho, Mkwasa alia kunyimwa bao...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI juzi mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, wakitoka sare ya tatu mfululizo dhidi ya Namungo FC kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, vinara wa ligi hiyo msimu huu, Yanga, jana walipata sare ya pili mfululizo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma, baada ya suluhu dhidi ya Ruvu Shooting.

Suluhu hiyo ni kwa Yanga ni kama imejicheleweshea ubingwa, kwani kama ingeshinda ingekuwa ni sawa na kuingia kwenye sebule ya nyumba iliyohifadhiwa kombe hilo.

Ni matokeo ambayo yanaifanya Yanga kufikisha pointi 56, ikiicha Simba kwa tofauti ya alama 13, kwani baada ya sare ya mabao 2-2 juzi dhidi ya Namungo ilifikisha pointi 43.

Ruvu Shooting ambayo iliipeleka mechi hiyo mjini Kigoma kuwa wenyeji, ilipiga hodi langoni mwa Yanga dakika ya pili tu ya mchezo kwa Rashid Juma kutoa pasi ya juu kwenda kwa Pius Buswita, ambaye aliingia ndani ya eneo la hatari, lakini alishindwa kupiga shuti na kubaki anazunguka, kutokana na kubanwa na mabeki wa Yanga ambao mwishowe waliufagia mpira.

Hatimaye Yanga ilifika langoni mwa Ruvu Shooting dakika ya 11, kutokana na faulo iliyopigwa na Saido Ntobazonkiza kwenda kwa Abobakar Salum, ambaye aliachia shuti lililopaa juu ya lango.

**Kinara wa mabao kwenye Ligi Kuu, Fiston Mayele angeweza kuipatia Yanga bao dakika ya 22 kama si mpira wa kichwa alichopiga kugonga mwamba wa juu na kurejea uwanjani. Ili kuwa ni krosi fupi iliyopigwa na Khalid Aucho.**

Ruvu Shooting ilijibu shambulio hilo dakika mbili baadaye, Saadat Mohamed alipowafungasha tela mabeki wa Yanga kwenye winga ya kushoto, kabla ya kuachia kombora kali lililopanguliwa na kipa Djigui Diarra na kuwa kona tasa. Saadat alipokea pasi hiyo kutoka kwa Rashid, mchezaji wa zamani wa Simba ambaye alikuwa kwenye kiwango cha juu kwenye mechi hiyo.

Hata hivyo, kulitokea kizaazaa kwenye lango la Ruvu Shooting dakika ya 49, baada ya krosi ya Kibwana Shomari kumkuta kipa Mohamed Makaka akiwa ametoka golini, lakini mabeki wa timu hiyo waliokoa na kumrudia kipa huyo alikokuwa amelala, akaudaka.

Mayele aligongesha tena mwamba dakika ya nne kabla ya mapumziko, ukiwa tena mwamba wa juu, lakini safari hii alipiga shuti kwa mguu wa kushoto, akiwa hatua mbili au tatu kutoka langoni mwa Ruvu Shooting.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, lakini Ruvu Shooting ikiendelea na mfumo wao ule ule wa pasi fupifupi wakionekana kuutawala mpira kwa muda wote wa mchezo, huku Yanga ambayo awali ilizidiwa na pasi za wenyeji wao, waliamua kubadilisha mfumo na kuanza kupiga pasi ndefu za juu zikielekezwa langoni.

Ikamwongeza na straika wengine wawili, Heritier Makambo na Chrispin Ngushi kwa lengo moja tu la kumsaidia Mayele na kuhakikisha mipira mirefu inaangukia golini, lakini wachezaji wa Ruvu Shooting, kina Abdurahman Mussa, Idd Mobi, Nathaniel Chilambo, pamoja na mchezaji Abdulswamad Kassim, wakiongozwa na kipa wao Mohamed Makaka walikaa imara, huku wakionekana kucheza kwa kiwango cha hali ya juu kuwafanya Yanga wapoteane.

Katikati ya kipindi cha pili, wenyeji walilazimika kucheza pungufu baada ya Rashid kuonyeshwa kadi nyekundu, zikiwa ni mbili za njano, kutokana na kuonekana kuchelewa kutoka baada ya kuumia, hivyo tafsiri ikaonekana ni kupoteza muda, lakini akitoa maneno ya lawama kwa mwamuzi.

Ruvu Shooting imefikisha pointi 22, ikiwa kwenye nafasi ya 14 ya msimamo, ikicheza mechi 21 mpaka sasa.

Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Mkwasa, baada ya mechi alilalamikia bao ambalo timu yake ilipata dakika za mwanzo za mchezo, ambalo lilikataliwa kwa madai mfungaji alikuwa ameotea.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >